CDAC NETWORK
communicating with disaster-affected communities

# Mwongozo wa Mandhari ya Vyombo vya Habari Nchini Kenya

Aprili 2024



# Shukrani

Hii ni sehemu ya mfululizo wa Miongozo ya Mandhari ya Vyombo vya Habari inayotolewa na Mtandao wa Communicating with Disaster Affected Communities (CDAC), kwa ushirikiano na usaidizi kutoka DW Akademie. Mwongozo huu uliandikwa na kuhaririwa kati ya Januari na Machi 2024.

Mtandao wa CDAC ungependa kumshukuru Stellar Murumba (mwanachama wa Kikundi cha Wataalamu wa CDAC), ambaye aliongoza utafiti, wanachama wa CDAC, na wengine katika vyombo vya habari, serikali, na mashirika ya kiraia nchini Kenya kwa michango yao. Shukrani za kipekee ni kwa FilmAid Kenya kwa usaidizi wao katika majadiliano na jamii za wakimbizi na wenyeji wa Dadaab, Kakuma na Kalobeyei, na kwa wale walioukagua mwongozo huu: David Omwoyo na Leo Mutisya (Baraza la Vyombo vya Habari nchini Kenya), Laura Wagenknecht na Sheila Mysorekar (DW Akademie), Joseph Ngugi (FilmAid Kenya), Abraham Mariita (Internews), Jamin Kusuania (International Rescue Committee), na Katie Ogwang, Godlove Kifikilo na Nicholas Midiwo (UNHCR).

DW Akademie

german cooperation
DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

**Nukuu inayopendekezwa:** CDAC Network (2024) *Mwongozo wa Mandhari ya Vyombo vya Habari Nchini Kenya* (www.cdacnetwork.org/media-landscape-guides/kenya-media-landscape-guide).

Picha ya jalada: Kusikiliza redio katika Dadaab Refugee Complex. Mpiga Picha: Internews | Flickr.

# Yaliyomo


**Shukrani** 2

**Mwongozo huu ni wa nani na kwa nini umeandaliwa sasa?** 4

**Mazingira ya ya kihistoria, kitamaduni na kisiasa** 5

- Historia ya ukoloni 6
- Kenya leo 6

**Muhtasari wa Vyombo vya Habari** 8

- Redio 8
- Televisheni 10
- Magazeti 11
- Mitandao ya kijamii 12
- Vyombo vya habari vya wakimbizi 13
- Mfano 15

**Mitindo katika mandhari ya vyombo vya habari** 16

- Lugha na lahaja 16
- Vizuizi vya kawaida vya ufikiaji 17
- Taarifa potofu na za uwongo 18
- Mapendeleo na uaminifu 19

**Vyombo vya Habari katika Makabiliano na Kujitayarishia Maafa** 20

- Jinsi ya kutumia mwongozo huu kujiandalia na kukabiliana na maafa? 21
- Mawasiliano ya njia mbili na jamii 22
- Fursa za maendeleo ya vyombo vya habari na mawasiliano katika mizozo 22

**Viambatisho** 24

**Maelezo ya Mwisho** 30

# Mwongozo huu ni wa nani na kwa nini umeandaliwa sasa?

Mwongozo huu unatoa taswira ya Mandhari ya Vyombo vya Habari, ikijumuisha habari dijitali na mitandao ya kijamii, redio, televisheni, magazeti na aina nyinginezo za kitamaduni za mawasiliano ya umma nchini Kenya. Mwongozo huu unajumuisha muktadha wa kimisingi, kisiasa na kitamaduni, ikijumuisha muhtasari mfupi wa hadhira, watayarishaji, mapendeleo ya vikundi mbalimbali na lugha zinazohusiana na vyombo vya habari. Mwongozo huu unagusia uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa kujieleza na miundomsingi ya vyombo vya habari. Mwongozo huu unachunguza hasa jukumu la vyombo vya habari, kazi ya ukuzaji wa vyombo vya habari, mawasiliano katika utayarishaji na ukabilianaji katika majanga, na unatoa mapendekezo ya mikakati madhubuti ikilenga waliotengwa na watu walioathiriwa na majanga. Kwa ujumla, dhamira yake ni kuwezesha mawasiliano ya kutegemeka, kuaminika na ya wakati unaofaa, hasa wakati wa majanga, na kukuza mazingira bora ya habari nchini Kenya.

Mwongozo huu unasasisha nyenzo ambazo zimepitwa na wakati au zenye upeo finyu, na unazingatia kwa kina mitindo ya matumizi ya habari ya wakimbizi. Mwongozo huu pia unatoa ushauri kuhusu vyombo vya habari vinavyofaa zaidi kwa mawasiliano katika demografia tofauti nchini Kenya. Tumia mwongozo huu kama sehemu ya kuanzia:

- Kuboresha uwezo wa watu kufikia habari bora zaidi kupitia ufikiaji mahsusi.
- Kushirikiana na vyombo vya habari kujitayarisha kukabiliana na maafa na kusaidia kujenga uwezo wa jamii kukabiliana na majanga.
- Kuongeza uwezo wa vyombo vya habari kuwasiliana na kushirikiana na vikundi tofauti, hasa wakati wa hali ya kuhama, mizozo na majanga [i].
- Kutumia ujuzi, mafahamiano na maarifa ndani ya sekta ya habari ya Kenya kwa ushirikishaji, ufikiaji na mawasiliano bora zaidi ya kijamii (rasilimali ambayo haijatumika ipasavyo).
- Kuhakikisha mkakati wako wa mawasiliano na ushirikishaji unaongozwa na jinsi watu tayari wanapokea taarifa na ni kina nani wanaowaamini.
- Kuokoa muda katika hali ya dharura kwa kuangalia ni nani anayetumia vituo gani vya habari, na uepuke kuwapuuza wanajamii fulani.

Utafiti ulifanywa ndani ya nchi na kuongozwa na kikundi cha marejeleo ambacho kilitoa mwongozo, ushauri wa kitaalam na uhakikisho wa ubora. Taarifa na takwimu zilikusanywa kupitia uhakiki wa maelezo yaliyopo, mahojiano ya wahojiwa wakuu (KII), mijadala ya vikundi lengwa (FGD) na tafiti za mtandaoni.[ii] Mahojiano na tafiti zilifanywa kwa kushirikiana na mdhibiti wa kitaifa wa vyombo vya habari, maafisa wa idara za serikali, wataalam wa vyombo vya habari (pamoja na wale wa kutoka vyombo vya habari vya wakimbizi na vya nchi jirani, na vyombo vya habari vya jamii), wasomi, wafanyakazi wa vyombo vya habari (watayarishaji na waandishi wa habari), mashirika ya maendeleo ya vyombo vya habari, mashirika ya kibinadamu, mashirika ya haki za binadamu na utetezi, waendeshaji kura za maoni, wanafunzi wa vyombo vya habari, Mashirika Yasiyo ya Serikali, wakimbizi na jamii wenyeji na umma kwa jumla.

# Mazingira ya ya kihistoria, kitamaduni na kisiasa

Sehemu hii inaangazia historia, utamaduni na nguvu za kisiasa zinazojenga mandhari ya sasa ya vyombo vya habari, namna na sababu mandhari haya yanayahudumia makundi mbalimbali. Sehemu hii inabainisha mapendeleo ya jamii na vikwazo vinavyowakabili wanapojaribu kufikia habari wanazohitaji.

Mandhari ya vyombo vya habari vya Kenya imejikita katika mbinu za mawasiliano za jadi, maarifa asilia na desturi za kitamaduni. Kutoka mbinu hizi hadi kuibuka kwa mifumo ya kidijitali, vyombo vya habari vya Kenya vimebadilika na kuwa kishindo madhubuti kinachobadilisha simulizi ya taifa hili.

Kanuni za kitamaduni zinasalia kuwa muhimu katika utamaduni wa leo wa mawasiliano ikiwa ni pamoja na kusimulia hadithi, simulizi za usemi, muziki na dansi, tambiko za mpito kama tohara na mazishi. Jamii za wachungaji huwasiliana kupitia sanaa ya kutazama kwa kutumia nakshi za mbao, ufinyanzi, na ushanga, zilizokita mizizi katika utamaduni wao, ili kusambaza habari. Katika baadhi ya maeneo ya mbali nchini Kenya, watu hutegemea mawasiliano ya usemi, viongozi wa maeneo husika na mikusanyiko ya kitamaduni kama sehemu muhimu ya mawasiliano, habari na ubadilishanaji habari. Mitindo ya kitamaduni sasa imebadilika, na usimulizi wa hadithi sasa unaweza kutokea hasa kupitia michezo ya kuigiza redioni, filamu halisia za televisheni, filamu, uigizaji na hata hafla za kitaifa zinazoangazia nyimbo na ngoma za kitamaduni. Hata hivyo, aina hizi za mawasiliano ni muhimu kwa urithi mnono wa kitamaduni wa nchi, na kwa hivyo haziwezi kutoweka kabisa, hasa kwani zinawaleta watu pamoja na kuhifadhi utambulisho wa jadi.

Kimsingi, njia za mawasiliano za kitamaduni zinaweza pia kuokoa maisha katika mizozo na hali za dharura. Ingawa si jambo geni, mfululizo wa mashambulio ya milingoti ya mawasiliano katika maeneo yanayoshambuliwa na Al-Shabaab katika Kaskazini Mashariki mwa Kenya karibu na mpaka wa Kenya na Somalia umethibitisha jambo hili hivi majuzi. Katika tukio la hivi majuzi mwezi Januari 2024, watu waliojihami waliharibu mlingoti ya mawasiliano katika Kaunti ya Mandera, takriban mwezi mmoja baada ya kuharibu mlingoti wa pekee katika eneo la Dasheg, Kaunti ya Wajir. Mashambulio kama haya pia yametokea katika Kaunti ya Garissa, inayowapa makazi wakimbizi wengi katika eneo la Dadaab Refugee Complex. Washambuliaji walitumia vilipuzi kuharibu mlingoti huu, na kusababisha ukatizaji mkubwa wa huduma za mawasiliano za eneo hili [iii]

> “...njia za kitamaduni za mawasiliano bado ni muhimu wakati aina nyingine [za mawasiliano] zinaharibika. Hatupaswi kutegemea tu mawasiliano ya kielektroniki.”
> (Mtoa habari mkuu, Shirika la usaidizi wa vyombo vya habari)

## Historia ya ukoloni

Utangazaji wa redio nchini Kenya ulianza mwaka 1927, wakati bado nchi ilikuwa koloni la Uingereza, kwa kuanzishwa kwa Shirika la Utangazaji la Afrika Mashariki (EABC), awali likisambaza habari za Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC). Matangazo ya Kiingereza yalianza mwaka 1928, yakiwalenga walowezi wazungu ambao walitafuta habari kutoka nchi zao na masuala ya kimataifa. Idadi ya watu asilia nchini haikuzingatiwa kuwa watazamaji wakuu hadi miaka kadhaa baadaye.[iv] Shirika la Utangazaji la Kenya (KBC), shirika la utangazaji linalomilikiwa na serikali lilikuwa kituo cha kwanza cha utangazaji cha televisheni nchini. KBC ilikabiliana na ushindani kutoka vituo vya televisheni vya kibinafsi na televisheni za setilaiti dijiti mwanzoni mwa miaka ya 1990 na 2000 mtawalia. Ingawa utangazaji umebadilika sana, KBC inasalia kuwa sehemu muhimu ya historia na mandhari ya taifa ya vyombo vya habari.

### Kenya leo

**Kenya ina idadi ya takriban watu milioni 54**.[v]Ni taifa la kidemokrasia lisilo na kidini lililo Afrika Mashariki linalopakana na Uganda, Tanzania, Sudan Kusini, Somalia na Ethiopia. Zaidi ya 85% ya Wakenya wanajitambulisha kuwa Wakristo, wakifuatiwa na Waislamu kwa 11%.[vi] Ni taifa la arobaini na tisa kwa ukubwa duniani kote, likiwa na jumla ya eneo la kilomita za mraba 580,367. Kenya ina uchumi mkubwa zaidi Afrika Mashariki[vii] huku bandari kubwa zaidi ya Mombasa ikiwa kitovu muhimu cha biashara kwa nchi jirani na nyinginezo kama vile Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

**Kenya ni nchi ya umoja yenye mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya kisiasa.** Ufuasi wa kisiasa mara nyingi umekuwa kwa misingi ya kikabila, ambayo imesababisha vurugu, kama ilivyozingatiwa kufuatia uchunguzi wa 2007 na 2012017. Katiba ya 2010 ilianzisha mfumo wa ugatuzi wa utawala ambao ulisajili kaunti 47 kwenye gazeti la serikali kugatua serikali ya kitaifa. Kaunti hizo zinaongozwa na magavana na naibu magavana waliochaguliwa, ambao wana mamlaka ya kuteua Kamati Tendaji za Kaunti, sawa na mawaziri wa kaunti, kulingana na idhini ya bunge la kaunti.

**Uhuru wa kujieleza na uhuru wa vyombo vya habari umewekwa katika katiba ya 2010.**[viii] Wanategemea sana hali ya kisiasa na kiuchumi iliyopo. Mnamo 2023, Kenya iliorodhesha nafasi ya 116/180 ulimwenguni katika faharasa ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Ulimwenguni.[ix] Kando na wasiwasi wa udhibiti na vikwazo, usalama wa waandishi wa habari katika mifuko ya nchi umekuwa ukining'inia kwenye mstari mwembamba. Wakati tunaandika, polisi walikuwa wamemkamata mshukiwa wa saba katika uchunguzi wa mauaji ya mwanablogu wa Kenya na mwanaharakati wa kisiasa huko Meru.[x] Kifo cha Daniel Muthiani kiliripotiwa kuhusishwa na msimamo wake mkali kuhusu masuala ya kijamii na kisiasa nchini na hasa kaunti yake. Alipatikana ameuawa kikatili katika hali isiyojulikana tarehe 17 Desemba 2023, huku mwanasiasa mkuu akidaiwa kuhusishwa na kifo chake.

**Wakuu wa kisiasa na kibiashara, pamoja na viongozi wa serikali, wamekuwa tishio kuu zaidi kwa vyombo vya habari nchini.** Baadhi ya wanahabari wameshambuliwa kimwili, vifaa vyao kuibiwa au kuharibiwa, hasa wakati wa maandamano ya umma na ukandamizaji unaofanywa na polisi. Mwezi Februari 2024, Baraza la Vyombo vya Habari nchini Kenya (MCK) - mdhibiti wa tasnia hii anayeidhinishwa kudumisha viwango vya maadili - lilishtaki serikali na biashara ya burudani jijini Nairobi kuhusu[vi]uvamizi kama huo dhidi ya wanahabari ambao walikuwa zamu wakiripoti kuhusu msako wa wauzaji haramu wa shisha.

**Kuna aina tatu za umiliki wa vyombo vya habari nchini Kenya: za umma, za kibinafsi na za kijamii.** Shirika la Utangazaji la Kenya (KBC) ni chombo cha habari kinachomilikiwa na serikali, kinachoendesha vituo vya televisheni na redio. Ndicho cha kwanza kabisa na miongoni mwa vyombo vya habari vilivyoenea zaidi nchini Kenya, kikiwa na mamlaka ya kutangaza habari kuhusu huduma za umma. Vyombo vya habari vinavyomilikiwa na watu binafsi ni pamoja na Nation Media Group, ambayo ni mojawapo ya makundi makubwa ya vyombo vya habari vya kibinafsi Afrika Mashariki na Kati, na imeorodheshwa katika Soko la Hisa la Nairobi. Ilianzishwa na Aga Khan na

inamiliki vituo vingi vya magazeti na vituo vya utangazaji, ikiwa ni pamoja na Daily Nation (gazeti), NTV (televisheni) na Nation FM (redio), awali iliyokuwa Easy FM. The Standard Group inafahamika kwa kuchapisha gazeti la The Standard, mojawapo ya magazeti ya kwanza kabisa nchini Kenya, na KTN, kituo maarufu cha televisheni. The Standard Group pia imeorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Nairobi. Royal Media Services (RMS): Inamilikiwa na S.K. Macharia, mchezaji mkuu katika nyanja ya vyombo vya habari nchini Kenya. Inaendesha runinga ya Citizen, ambayo ni mojawapo ya vituo maarufu vya televisheni nchini Kenya, na vituo kadhaa vya redio, ikiwa ni pamoja na Radio Citizen, kituo maarufu cha redio nchini. Mediamax Network inamilikiwa na familia ya Kenyatta na inaendesha K24 TV, People Daily (gazeti la kitaifa lisilolipishwa), na vituo kadhaa vya redio. Redio Africa Group inamiliki gazeti la The Star na vituo kadhaa vya redio kama Kiss FM, Classic 105 na Radio Jambo. Baada ya kutathmini tovuti 35 za habari nchini Kenya zinazotoa habari za uongo, utafiti wa hivi majuzi uligundua: "Ukadiriaji wa jumla (wa Kenya) … unaathiriwa na mapungufu ya kiutendaji, hasa kuhusu uwazi wa habari kuhusu wamiliki halisi au wanuafaika wa faida za tovuti, vyanzo vyake vya ufadhili na sera nyingine za uendeshaji na uhariri." [xii]

**Vituo kumi vya habari vinatawala mandhari ya media.** Vyote ni wanachama wa Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari nchini Kenya. Umiliki ni muhimu kwani unaweza kuathiri uhuru wa wahariri na msimamo wa vyombo vya habari, hasa katika masuala ya kisiasa na kijamii na kiuchumi.

**Vyombo vya habari lazima vizalishe faida.** Hii inakuza mtindo wa kutegemea kupita kiasi wafadhili wachache wakuu wa matangazo na maudhui yaliyofadhiliwa. Vituo vingi vinadaiwa kuhangaika kifedha, ikithibitishwa kupitia ripoti za kucheleweshwa kwa mishahara au kutolipa mishahara au kulipa viwango vya chini sana vya mishahara ya wafanyakazi.[xiii]Mwezi Januari 2024, vyombo vya habari vya Kenya vililalamikia kutolewa kwa matangazo ya 'MyGov' kwa shirika moja tu la vyombo vya habari.[xiv] Wizara ya TEHAMA, Ubunifu na Masuala ya Vijana ilitoa notisi kwa Makatibu Wakuu wote, Wakurugenzi Wakuu wa Mashirika ya Serikali, Tume Huru na Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu vya Umma, ikionyesha kuwa matangazo yote sasa yatachapishwa na kusambazwa na Gazeti la Star pekee. Uamuzi huu unaashiria mabadiliko makubwa kutoka kwa utaratibu wa awali, ambapo matangazo ya serikali yalichapishwa na kusambazwa kupitia MyGov na magazeti manne ya kila siku: Nation, Standard, Star na People Daily. Kwa hivyo, kandarasi hiyo ya miaka miwili itasababisha Daily Nation, The Standard na The People Daily kupoteza mamilioni ya pesa.

**Kuvurugwa kisiasa, udhibiti na kupungua kwa mapato yote ni mambo ambayo yanachangia mazingira magumu ambayo vyombo vya habari vya Kenya hufanyia kazi.** Vyombo vya habari vinakabiliana na shinikizo kutoka kwa waendeshaji wa kisiasa, wakati X ya Kenya imeibuka kuwa jukwaa lililo na ongezeko la ufahamu wa kisiasa, jambo ambalo linadhihirisha vipengee vingi vya Mandhari ya Vyombo vya Habari nchini. Licha ya vikwazo, vyombo vya habari vinasalia kuwa njia muhimu ya usambazaji wa habari, uwajibikaji na udumishaji maadili ya kidemokrasia. Mwezi Machi 2024, Kikundi Kazi cha Sekta ya Vyombo vya Habari nchini Kenya kilichojumuisha vyombo tofauti vya habari na wanahabari (yaani, Muungano wa Wanahabari wa Kenya, Chama cha Wahariri wa Kenya, Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari, jamii ya Wahariri wa Afrika Mashariki, Chama cha Wanawake wa Vyombo vya Habari nchini Kenya n.k.) kiliongoza wito wa kuchukua hatua dhidi ya kuvurugwa na serikali katika mandhari ya vyombo vya habari nchini Kenya. Walitoa wito wa mshikamano kati ya wanahabari wote, vyombo vya habari na wadau wa vyombo huru vya habari kuungana kutetea haki zilizopatikana kwa juhudi kubwa ili kupata uhuru wa vyombo vya habari.

**Sheria ya Wakimbizi ya 2021 sasa inatoa mfumo wa kisheria unaojumuisha haki za uhuru wa kujieleza, uhuru wa kuzungumza na vyombo vya habari na kupata habari kwa wakimbizi na wanaotafuta hifadhi.** [xv] vyombo vya habari vinatakiwa kuchukua hatua kwa uwajibikaji ili kuepuka kuwasisimua au kuwanyanyapaa zaidi wakimbizi na wanaotafuta hifadhi. Sheria hizo pia zinaonyesha miongozo ya utangazaji kuhusu masuala ya wakimbizi, zikisisitiza umuhimu wa usahihi, haki, na kuheshimu utu wa wakimbizi. Wanahabari wanahimizwa kuripoti kuhusu masuala ya wakimbizi kwa namna ambayo inakuza uelewa na ufahamu kwa wakimbizi na watafuta hifadhi. Isitoshe, sheria zinakataza usambazaji wa taarifa za uongo ambazo zinaweza kuchochea chuki au ubaguzi dhidi ya wakimbizi na watafuta hifadhi. Ukiukaji wa sheria hizi unaweza kusababisha adhabu za kisheria

# Muhtasari wa Vyombo vya Habari

Redio (77%) na TV (74%) ndiyo mifumo mikuu ya vyombo vya habari katika mikoa yote (isipokuwa mkoa wa Kaskazini Mashariki ambako intaneti inaongoza), ikifuatiwa na mitandao ya kijamii na tovuti (57%), magazeti (7%) na familia/marafiki/wafanya kazi wenza.[xvi]

## Redio

**Redio inasalia kuwa mguzo ya kupokea habari nchini Kenya.** Kuna vituo 303 vya redio vilivyoidhinishwa: 212 kibiashara FM redio, 78 jumuiya[xvii] .Vituo vya redio vya FM na vituo 13 vya umma vya FM[xviii] Kati ya hizi, 291 walikuwa wakitangaza kikamilifu. Vituo vingi pia vina uwepo mtandaoni, huku vingine vikitoa huduma za utiririshaji wa moja kwa moja, na kuviwezesha kufikiwa kimataifa na watu wanaoishi nje ya nchi. Asilimia 66 (66%) ya kaya zinamiliki redio yenye umiliki mkubwa zaidi mijini (71%) ikilinganishwa na maeneo ya vijijini na pembezoni (62%).[xix] Licha ya kupungua kwa hivi majuzi kwa umiliki wa redio zinazojitegemea huku watu wengi wakipata ufikiaji wa vifaa vilivyounganishwa na redio kama vile simu za rununu, vicheza sauti, magari, kompyuta na saa za kengele, redio inasalia kuwa njia iliyoenea zaidi ya udhihirisho wa media kwa wanawake wote (62%) na. wanaume (71%).[xx] Wengi pia wanasikiliza redio kupitia seti za TV, kompyuta za mkononi na utiririshaji mtandaoni. Kuongezeka kwa huduma za utiririshaji wa video na mabadiliko ya mapendeleo miongoni mwa vizazi vichanga ni mambo mengine yanayosababisha kupungua kwa umiliki wa redio huru. Redio huvutia kiasi makundi ya umri wa juu zaidi wa miaka 35+ (50.1%), ikilinganishwa na makundi machanga zaidi ya umri wa miaka 15 na 24 (20.4%).

**Radio Citizen ndicho kituo cha redio kinachosikilizwa zaidi**, ikichukua asilimia 14.9%[xxi] ya wasikiliazako redio nchini Kenya, ingawa imeshuka kutoka 18% mwaka uliopita, kulingana na GeoPoll Inc. Radio Maisha na Radio ya Standard. Kipindi cha Radio Jambo cha Africa Group kilifuata kwa karibu na 10.5% na 9.2% ya watazamaji wa asubuhi. Vituo vya Classic FM (8.2%) na Milele FM (6.1%) vilifunga orodha ya tano bora (Angalia Kiambatisho cha 5 upate maelezo zaidi).

**Usikilizaji redio** ni wa viwango vya juu zaidi katika Nyanza Kusini (85%), mikoa ya Ziwa na Bonde la Ufa kwa 84% na 83% mtawalia, na eneo la Magharibi (82%). Viwango vya chini zaidi vya usikilizaji vilirekodiwa katika eneo la Kaskazini Mashariki. Viwango vya usikilizaji katika maeneo ya vijijini (82%) viko juu kuliko mijini (67%). **Nyakati za juu za kusikiliza** ni 7am na 9am, ambayo huvutia wasikilizaji wengi wa watu milioni 27.[xxii] Hii inapendekeza kwamba watu wengi husikiliza wakati wa safari zao za asubuhi au wanapoanza siku yao ya kazi. Kuna idadi kubwa zaidi ya wasikilizaji Jumapili na Jumamosi asubuhi ikilinganishwa na siku za wiki. Redio sasa ina kipengee cha kuwezesha mawasiliano ya njia mbili. Wasikilizaji wanaweza kushiriki na kuwasiliana na waandalizi wa vipindi kwa kutuma SMS au kupiga simu wakati wa vipindi vya moja kwa moja au vipindi vya matukio ya redioni. Hata hivyo, kama ilivyo kwa mbinu yoyote ya habari, redio ina mapungufu. Watu walio katika maeneo ya mbali na yaliyotengwa yenye masafa duni ya redio, watu wenye ulemavu wa kusikia na wale wanaofanya kazi wakati wa upeperushaji, wanaweza kutengwa.

**Katika mazingira ya wakimbizi, watu walitufahamisha kuwa redio ni chanzo kikuu cha habari**, ikifuatwa na mitandao ya kijamii, viongozi wa kijamii, huduma ya kutuma SMS nyingi, mabango, brosha na televisheni. BBC Somali ni kituo kinachopendelewa zaidi na Wasomali wa umri mkubwa zaidi kambini Dadaab. Nyakati za kilele za usikilizaji zilikuwa tofauti na za wasikilizaji wa nchi nzima, huku nyakati za jioni zikipendekelewa, za kati ya saa kumi na moja na saa mbili jioni (5pm na 8pm) kwa wakimbizi na jamii wenyeji, kulingana na takwimu kutoka DW Akademie. Usikilizaji wa redio katika kambi hizo ulikuwa wa chini zaidi katika nyakati za kati ya saa mbili na saa tano asubuhi (8am na 11am), ilhali wakati huu wa kilele kwa usikilizaji wa redio nchini kote.


Wakimbizi wakiwa Kakuma

ZORIAH | FLICKR

**Radio Gargaar**[xxiii] **sasa ndicho kituo pekee cha redio cha FM kinachotumika katika kambi ya Dadaab na kinaaminika** kusambaza taarifa za kuaminika. Huku kikishirikiana na kituo chanzi cha Star FM katika eneo la Eastleigh Nairobi, kinachomilikiwa na Star Media Development Centre, "Gargaar" ni jina linalomaanisha usaidizi. Kinawaunganisha watu walioathiriwa na majanga na mashirika ya misaada ya kibinadamu.[xxiv]

**Kule Kakuma, Redio Ata Nayece**[xxv] **na RREF FM zilijitokeza kama vyombo vya habari maarufu zaidi vya wakimbizi.** Vina sehemu ambapo wanawaalika wataalam mbalimbali ikiwa ni pamoja na wakimbizi, watafuta hifadhi, wataalam wa masuala ya wakimbizi, wafanyakazi wa misaada kwa wakimbizi, maafisa wa serikali na jamii wenyeji kuifahamisha jamii kuhusu masuala muhimu yanayowahusu. Sauti ya Amerika ilizindua vituo viwili vya FM vinavyoongozwa na wakimbizi kuwahudumia wakimbizi na watafuta hifadhi kambini Dadaab na Kakuma mwaka 2020, ingawa havijakuwa maarufu sana au kutumiwa sana na mawakala katika kambi hizi.



## Televisheni

**Kwa sasa kuna vituo 346 vya TV vilivyo na leseni nchini Kenya.**[xxvii] Televisheni bila malipo ya kibiashara ni 337 na vituo vya Televisheni visivyo na jamii ni tisa. Usahili wa Televisheni Dijitali, Televisheni ya Setilaiti na Kebo ulifikia milioni 4.5, milioni 1.8 na 64,631, katika kipindi cha tarehe 1 Julai na 30 Septemba 2023, mtawalia. Nusu ya familia zote nchini Kenya zinamiliki televisheni. Watazamaji wa televisheni ni wengi zaidi mijini, ikilinganishwa na mazingira ya vijijini. Matumizi ya juu zaidi ni Mashariki ya Juu (87%), Kati (83%) na Nairobi (80%). Kaskazini Mashariki (53%), sawa na usikilizaji redio, ilikuwa na watazamaji wachache zaidi wa televisheni.

**Citizen TV inaongoza kwa kuwa na watazamaji wengi zaidi kitaifa k**wa asilimia 38% (sawa na kituo tawi lake la Radio Citizen kinachomilikiwa na Royal Media Services). NTV inashika nafasi ya pili kwa 13%, ikifuatiwa kwa karibu na KTN Home, KBC, na haswa Inooro TV (8%), ikiwakilisha maudhui ya lugha za Kikuyu.[xxviii] Hasa, data ya GeoPoll (2022) inaonyesha Al Jazeera kama kituo pekee cha televisheni cha kimataifa katika 10 bora, katika robo ya kwanza ya mwaka huo.

**Wanaume wanatawala utazamaji wa vituo vyote vya televisheni**, isipokuwa Inooro TV, ambayo ina hadhira ya juu kidogo ya wanawake kwa asilimia 56%. Watazamaji wachanga kati ya umri wa miaka 15 na 24 wanapendelea K24, NTV na Kiss Tv,xxix[xxix] ambayo imefungwa tangu wakati huo. Maisha Magic East, KTN News, na Al Jazeera, kwa upande mwingine, zilikuwa chaguo maarufu zaidi kwa watazamaji wa miaka 25-34. Citizen TV, Inooro TV na KBC zilipendelewa na watu wa umri wa miaka 35 kwenda juu. Watoto wa chini ya miaka 14 walikadiria Akili Kids TV kuwa kituo maarufu zaidi, kulingana na takwimu za GeoPoll ya 2024.

**Kipindi kinachotazamwa zaidi ni taarifa za habari za Citizen TV za saa tatu usiku (9pm),** ambacho hufikia kilele Jumanne kwa asilimia 33.2%. Vituo vingine vilivyotazamwa zaidi wakati huo ni NTV ikifuatiwa na KTN Home na KTN News. TV 47 iliibuka kama mshindani mashuhuri, huku asilimia 3% ya watazamaji wakiitazama wakati huu (angalia viambatisho upate maelezo zaidi).

**Vizuizi vikuu vya utazamaji wa TV** ni gharama kubwa, za kununua televisheni, umeme na usajili au leseni za uendeshaji kwa wamiliki. Kwa hivyo, Televisheni Isiyolipidhwa (FTA) inapata watazamaji wengi zaidi ikilinganishwa na televisheni ya kulipia, ingawa aina hii ya pili ni maarufu zaidi mijini kuliko vijijini. Makampuni kama Mkopa yanajitahidi kuziba pengo la umiliki wa televisheni kwa kuwapa watumiaji fursa ya kupata televisheni za bei nafuu na inatoa machauo ya umeme wa jua kupitia ununuzi wa kukodisha, na hivyo kuwapa njia mbadala watu ambao hawajaunganisha umeme. Televisheni ina vipengele vya kutazama na kusikiliza, na kwa hivyo kuifanya kuwa fanisi kwa mawasiliano hasa pale ambapo lugha au ulemavu unakuwa kikwazo kwani mtu anaweza kubaini maana ya kile anachokiona. Televisheni hutoa mawasiliano ya njia mbili.

**Katika mazingira ya wakimbizi**, televisheni si chombo cha habari kinachotumiwa sana kwa sababu za ufikiaji na gharama zake. Star TV inayomilikiwa na Star Media Development Center ndicho kituo pekee cha televisheni nchini ambacho kwa kiasi fulani huonyesha vipindi vya televisheni vinavyowafaa wakimbizi. Kinapeperushia kutoka jumba la BiHi Towers jijini Nairobi CBD.

## Magazeti



ERIK HERSMAN | FLICKR


**Kuna takwimu chache kuhusu idadi ya jumla ya magazeti yenye leseni nchini Kenya, utafiti uliofanywa kwa ajili ya kuandika mwongozo huu unaangazia angalau magazeti 17 yaliyo na leseni ambayo yanachapishwa.** Baraza la Vyombo vya Habari nchini Kenya pia hutoa takwimu za kila mwaka za magazeti yanayosomwa mara nyingi zaidi nchini. Gazeti la Daily Nation (53%) ndilo linalosomwa zaidi, likifuatiwa na Standard (22%) na Taifa Leo (15%). Magazeti ya Daily Nation na Taifa Leo ni machapisho ya Nation Media Group (NMG) , huku Taifa Leo likiwa chapisho la pekee la kituo kikubwa linaloandikwa kwa Kiswahili nchini. Nation Media Group pia inamiliki gazeti pekee la kina la michezo la Kiswahili nchini liitwalo Mwanaspoti, ambalo huangazia habari za michezo za nchini, kikanda na kimataifa. Machapisho mengine ni pamoja na The Star, Sunday Nation ya Nation Media Group, Business Daily, Taifa Leo na People Daily. Majarida makuu ni pamoja na Parents, Drum na True Love. Mahojiano ya wahojiwa wakuu na ya utafiti yaliyofanywa kwa ajili ya utafiti huu yalibainisha kuwa sababu maarufu zaidi za kuchagua gazeti au jarida fulani ni pamoja na uaminifu wa gazeti husika, uwiano na maadili ya kibinafsi, na burudani ya maudhui.

**Taarifa za kuchapishwa zina kikomo katika uwezo wake wa kufikia nchi nzima, lakini inaweza kuathiri masuala ya kitaifa.** 70% ya umma hawasomi magazeti, iwe ya muundo halisi au wa kidijitali.[xxx] Kuna vikwazo katika kufikia sehemu za mbali za nchi. Hata hivyo, Washiriki katika utafiti wa mwongozo huu, hasa wale wanaofanya kazi katika vyombo vya habari na mashirika ya misaada ya kibinadamu, walitaja magazeti ya Daily Nation na Standard kuwa magazeti wanayopenda zaidi kwa sababu ya maelezo ya kina ambayo hayapatikani katika aina nyingine za vyombo vya habari. Uwezo wa taarifa za kuchapishwa wa kutoa makala za muundo mrefu, mahojiano na uchanganuzi ni mchango muhimu wa kuushirikisha umma na mara nyingi huongeza ufahamu wa umma kuhusu masuala.

**Mawasiliano ya pande mbili kupitia vyombo vya habari vya kawaida vya kuchapisha ni kupitia** barua kwa mhariri au uandishi wa maoni. Pia inabakia kuwa mchakato wa ushiriki wa wasomi, usioweza kufikiwa na wengi. Jamii zilizotengwa zina ufikiaji mdogo wa habari za kuchapishwa kwani mara nyingi ni ghali na hazipatikani kwa urahisi katika maeneo yao. **Ni kituo kimoja tu cha gazeti linaloangazia masuala ya wakimbizi lililopatikana**: Jarida la 'The Refugee' lililochapishwa na FilmAid Kenya kwa usaidizi kutoka kwa wafadhili.

> "Ndiyo, ninapata habari ya kuchapisha, ikiwa ni pamoja na magazeti na majarida. Tuna mandhari anuwai na ya kuvutia ya uchapishaji magazeti, huku machapisho ya nchini na kimataifa yakipatikana. Jambo hili linasababishwa na kiwango cha juu cha watu wanaojua kusoma na kuandika, msisitizo mkubwa kuhusu uhuru wa kujieleza, na aina mbalimbali za maslahi na maoni yanayotolewa katika habari za kuchapisha. Ni vyema kutambua kwamba habari za kuchapisha bado zina jukumu muhimu katika mandhari ya habari na mawasiliano ya Kenya pamoja na habari digitali."
> (Mtoa taarifa muhimu, INGO)

## Dijitali




**Wakenya wengi hutumia habari digitali** (aina yoyote ya maudhui ambayo yanaandaliwa na kusambazwa kielektroniki). Magazeti ya kuchapisha yanazidi kupewa changamoto na magazeti pepe, ambayo yanaandaliwa na mashirika yale yale ya utangazaji, na yana wasomaji wengi zaidi katika maeneo ya Nairobi na Magharibi mwa Kenya.[xxxi] Rejelea kiambatisho upate maelezo zaidi kuhusu tovuti za habari zinazotembelewa mara nyingi zaidi. Mifumo ya kidijitali, kama vile mitandao ya kijamii, tovuti, huduma za utiririshaji, programu za simu, machapisho ya kidijitali, na tovuti za habari za mtandaoni, huwezesha usambazaji wa haraka wa taarifa. Mifumo hii hutoa ufikiaji wa taarifa za moja kwa moja, maoni ya wataalamu, nyenzo za elimu na burudani ya kielimu. Habari dijitali pia hurahisisha ushiriki ingiliani kupitia maoni, warsha na mijadala ya mtandaoni.

**Utumiaji wa habari dijitali umechochewa kwa kiasi kikubwa na kuenea kwa simu za mkononi, teknolojia, na kasi ya intaneti.** Umiliki wa kompyuta unasalia kuwa mdogo kitaifa katika asilimia 11 tu ya kaya, ambapo 4% tu ndizo ziko vijijini, lakini bidhaa inayopatikana zaidi katika kaya za Kenya ni simu ya rununu yenye umiliki wa 94%.[xxxii] Mnamo 2023, jumla ya idadi ya simu za rununu ilifikia milioni 64.7, na milioni 32.6 na milioni 32.1 zikiwa simu mahiri na zinazoangazia simu mtawalia.[xxxiii]

**Kufikia Januari 2024, watoa huduma watano wa mtandao wa simu wamepewa leseni nchini Kenya.**[xxxiv] Kwa upande wa sehemu ya soko katika usajili wa huduma, Safaricom PLC inaongoza kwa 61.9% ikifuatiwa na Airtel Networks Kenya Ltd kwa 32.7%. Telkom Kenya Ltd, Finserve (Equitel) Ltd na Jamii Telecommunications Ltd zinafuata kwa 2.5%, 1.6% na 1.3% kwa mpangilio huo.[xxxv] Data ya rununu na Broadband[xxxvi] huduma zilifikia alama milioni 49.3 katika robo ya kwanza ya 2024 huku mtandao wa 4G ukionekana kupokelewa zaidi kwa watumiaji milioni 23.9.

Katika mazingira ya wakimbizi, watoa huduma wale wale wa mtandao wa simu hutumiwa. Utumiaji wa intaneti ni mkubwa Kaskazini Mashariki mwa Kenya, maana kwamba wakimbizi katika kambi ya Dadaab, wenye uwezo wa kufikia simu mahiri na vifaa vingine vilivyounganishwa kwenye mtandao, wanaweza pia kufikia habari digitali wanayoipenda, ingawa hakuna takwimu mahususi zinazoonyesha utumiaji mahsusi kwa wakimbizi na watafuta hifadhi.

## Mitandao ya kijamii

Mageuzi ya haraka ya mitandao ya kijamii yamebadilisha kwa kiasi kikubwa mandhari ya vyombo vya habari, yakipelekea njia mpya za mawasiliano, usambazaji wa habari na ushiriki wa umma. Washiriki wa mwongozo huu walitaja mitandao ya kijamii kama mtoaji wao mkuu wa taarifa (sio habari tu) na waliripoti kuwa majukwaa ya mitandao ya kijamii yaliyotumiwa zaidi (kwa mpangilio wa umaarufu wake) yalikuwa.

- WhatsApp
- Facebook
- X (iliyokuwa Twitter)
- Instagram
- Tik Tok
- YouTube
- Telegram

Hii inalingana kwa jumla na takwimu rasmi za hivi majuzi.

| Mitandao mikuu ya kijamii | Matumizi ya mitandao ya kijamii mwaka 2022 |
|---|---|
| Facebook | 23% |
| WhatsApp | 22% |
| YouTube | 11% |
| X | 8% |
| Tik Tok | 7% |

**Mitandao ya kijamii huwezesha ukuzaji wa habari kupitia washawishi** na mashirika, na imewawezesha watu kujitosa kwa usawa katika uandishi wa habari wa kiraia, na hivyo kupanua wigo wa habari zilizojanibishwa kutokana na matukio ya kibinafsi. Mitandao ya kijamii imekuwa muhimu kuangazia majanga yanapotokea, na kushiriki habari ambazo hazijachujwa, na zinazoenea kwa haraka. Taarifa huenea haraka kwenye majukwaa haya, na kasi ya ushiriki wa umma pamoja na kushiriki rasilimali miongoni mwa mashirika ya serikali au makampuni hufanyika kwa haraka sana. Hii ni kwa sababu ya asili ya watu ya kutaka kushiriki habari, pamoja na kasi ya mtandao iliyoboreshwa.

**Mifumo ya mtandaoni pia inabadilisha shughuli za kuzalisha mapato za mbali na za kidijitali** kwani watumiaji wanaweza kuchuma mapato kutokana na vituo vyao vya mitandao ya kijamii ili kujipatia riziki kulingana na maudhui wanayotayarisha na kushiriki kwenye mitandao ya kijamii. Kenya pia ni makao makuu ya afisi ya Meta Group Kusini mwa Jangwa la Sahara jijini Nairobi, ambapo udhibiti wake mwingi wa maudhui ya majukwaa ya kampuni hiyo kubwa ya mitandao ya kijamii hufanyika. Hatari za uchumi wa mtandaoni nchini Kenya zinaendelea kurekodiwa na wanahabari. Kuna juhudi zinazoendelea za kuboresha haki za wafanyakazi wa udhibiti wa maudhui ya kidijitali kutokana na hatari hizi.[xxxviii]

## Vyombo vya habari vya wakimbizi

**Vyombo vya habari vya wakimbizi vinaendeshwa na kusimamiwa na wakimbizi na jamii wenyeji ili kuendesha masimulizi yao wenyewe**. Mara nyingi vyombo hivi hukua kutokana na hitaji la mawasiliano na upashanaji habari miongoni mwa jamii nyingi. Vyombo vya habari vya wakimbizi huchukua aina mbalimbali, kuanzia vituo vya redio vya muda hadi magazeti/majarida ya nyanjani, mitandao ya kijamii na majukwaa ya kidijitali. Kutoka Dadaab hadi Kakuma, Kalobeyei hadi Eastleigh (eneo la wakimbizi la Somalia mjini Nairobi), idadi kubwa ya vyombo hivi vya habari inaendeshwa na mashirika yanayoongozwa na Wakimbizi (RLO) ambayo yanafanya kazi katika tasnia ya habari na ubunifu. FilmAid Kenya, GIZ na DW Akademie ni baadhi ya mashirika mengine ambayo yameshiriki katika kujenga mandhari ya vyombo vya habari vya wakimbizi nchini Kenya katika masuala ya maendeleo ya vyombo vya habari. Mashirika kama vile FilmAid Kenya yamekuwa mstari wa mbele katika kuwajengea uwezo wakimbizi, watafuta hifadhi na jamii zinazowakaribisha katika uandishi wa habari na vipindi vya mafunzo ya filamu, ambao nao wameunda RLO zinazotumika katika kambi. Mifano ya RLO hizi ni pamoja na Sound for Life, Jiba Pictures Media House, Kakuma Ventures, Moris Studio, MonyQadow na Kasinde Films.

**Hakuna waendeshaji wa vyombo vya habari huru na endelevu za kibiashara wanaolenga jamii zilizohamishwa makwao.** Miundo hii hatimaye inategemea usaidizi kutoka nje kutoka kwa wafadhili, UNHCR, na washirika waendeshaji katika kambi ambao hutoa ufadhili, kulipia vipindi vya redio vinavyotumika kusambaza taarifa muhimu.

**Vyombo vya habari vya wakimbizi vina jukumu muhimu katika kutoa onyo la mapema na uratibu wa u**toaji misaada na usaidizi. Vyombo hivi pia vina jukumu kubwa katika kusambaza habari za matumaini na uthabiti sio tu kwa wakimbizi na watafuta hifadhi, bali pia kwa jamii wenyeji, katika mazingira ya wasiwasi kwa wale waliohamishwa makwao kufuatia majanga. Mifumo hii pia hujitahidi kutoa utetezi na uhifadhi wa kitamaduni miumo kwa wakimbizi wa kutoka nyanja mbalimbali. Hata hivyo, mifumo hii inakabiliwa na changamoto kama vile rasilimali chache na ukosefu wa usalama.


Lakini, hakukuwa na marejeleo yaliyopatikana kuhusu miongozo ya vyombo vya habari vya wakimbizi nchini, ingawa vinafanya kazi katika mazingira tofauti kabisa na vyombo vya habari vikuu na vya jamii. Ilikuwa ngumu pia kugawanya takwimu ili kuonyesha waandishi wa habari, ambao pia ni wakimbizi, wanaofanya kazi katika sekta ya vyombo vya habari kwa jumla.

**Maarifa kutoka kwa FGD katika kambi za wakimbizi yanaangazia** vipengele mbalimbali vya utumiaji wa vyombo vya habari, viwango vya kujua kusoma na kuandika, vipengee vya kitamaduni, na mitindo ya mitandao ya kijamii katika mandhari ya vyombo vya habari vya wakimbizi.

Matokeo muhimu yaliyojumuishwa:

1. **Utumiaji habari:** Wakimbizi katika Kambi za Wakimbizi za Dadaab na Kakuma, na Makazi Jumuishi ya Kalobeyei kimsingi hutegemea redio kama chanzo chao kikuu cha habari. Redio zinapatikana kwa wingi na kwa bei nafuu, na kuzifanya ziwe chaguo linalopendelewa kwa habari na burudani. Televisheni pia ni maarufu lakini haipatikani kwa urahisi kwa sababu ya vikwazo vya kigharama na miundomsingi. Habari zilizochapishwa hazitumiki sana, huku magazeti na majarida yakitumika mara chache zaidi.
2. **Viwango vya uwezo wa kusoma na kuandika:** Ingawa viwango vya kujua kusoma na kuandika vinatofautiana kati ya wakimbizi, kuna mtindo wa jumla wa viwango vya chini vya kusoma na kuandika ikilinganishwa na watu wa jamii wenyeji. Hii huathiri aina za vyombo vya habari vinavyotumiwa, huku redio ikiwa inafikiwa zaidi na wale walio na viwango vya chini vya kusoma na kuandika.
3. **Tofauti fiche za kitamaduni:** Vipengele vya kitamaduni vina jukumu kubwa katika utumiaji na mapendeleo ya habari. Kwa mfano, vituo vya redio vya jamii vinavyotangaza katika lugha za kienyeji vinathaminiwa sana kwa vile vinawasilisha maudhui ya kitamaduni na kutoa maudhui ambayo yanawahusu hadhira. husika Washiriki wa mwongozo huu pia walisema kwamba kabla ya kushirikisha jamii katika ngazi mbalimbali, viongozi wa jamii wana uwezo bora zaidi kueleza vipengele vyao vya kitamaduni kwa ajili ya matokeo bora, ili kukubalika na jamii.
4. **Vipengee vya mitandao ya kijamii:** Ingawa ufikiaji wa intaneti na mitandao ya kijamii ni mdogo katika kambi za wakimbizi, wale wanaoweza kuufikia mara nyingi hutumia majukwaa kama Facebook na WhatsApp ili kuwasiliana na familia na marafiki, na pia kupata taarifa na habari. Hata hivyo, kuna changamoto kama vile vikwazo vya muunganisho na ukosefu wa vifaa.
5. **Imani katika vyombo vya habari:** Imani katika vyanzo vya habari inatofautiana, na wakimbizi mara nyingi hutegemea mawasiliano ya usemi na viongozi wa jamii, ambao wamewachagua, kwa habari, ingawa usambazaji unaweza kuchelewa. Vyanzo vinavyoaminika ni pamoja na vituo vya redio ambavyo vinaonekana kuwa kutoegemea upande mmoja, na vinavyoripoti kwa umainifu. Vyombo vinavyowaalika wanajamii na wataalam kutoka mashirika tofauti kuzungumza kuhusu masuala muhimu pia vinaaminika.
6. **Mahitaji ya taarifa:** Wakimbizi walisema wanahitaji habari zaidi kuhusu haki za kisheria, huduma ya afya, elimu, na fursa za kujikimu. Kuna hitaji la maudhui anuwai na faafu zaidi ambayo yanashughulikia mahitaji haya.[xxxix]
7. **Changamoto:** Ufikiaji mdogo wa habari, vizuizi vya lugha, na habari potofu ni changamoto kuu zinazowakabili wakimbizi katika juhudi za kufikia na kutumia vyombo vya habari. Katika Kambi ya Kakuma, ambako angalau mataifa 25 yanawakilishwa, bado ni lugha chache sana zinazopatikana ambazo zinatumika katika kusambaza habari na mawasiliano ya serikali na mashirika. Pia kuna haja ya mafunzo zaidi katika ujuzi wa vyombo vya habari na mawasiliano.

Mawazo haya yanaangazia umuhimu wa kuelewa tabia mahususi za utumiaji wa vyombo vya habari, viwango vya kusoma na kuandika, na miktadha ya kitamaduni ndani ya jamii za wakimbizi ili kushiriki kikamilifu na kuwasiliana nao kabla ya majanga au maafa, yanapoendelea na baadaye.




FILMAID KENYA

## Mfano

**“Sikika”** ni mradi wa kuboresha ufikiaji wa taarifa kwa wakimbizi na jamii zinazowakaribisha, na kukuza mazungumzo kati ya jamii mbalimbali na mashirika ya misaada ya kibinadamu, katika kambi ya Kakuma kupitia DW Akademie.

"Sikika" hushirikiana na wanajamii 290 (wenyeji na wakimbizi), ambao wamefunzwa na kupewa redio ili kushiriki maudhui ya timu ya Sikika yaliyotolewa kwa maoni ya wanajamii. Wao huandaa vipindi vya kusikiliza ndani ya jamii na kurekodi miitikio ya washiriki. Muda huu huwapa maoni Wanahabari wa jamiina mashirika ya misaada ya kibinadamu kwa muda mrefu. WhatsApp ya Sikika huendeleza mazungumzo haya.

Tofauti na vituo vingine vya redio ni kwamba maudhui yake yanatolewa na Wanahabari vijana wa jamii kutoka kwa wakimbizi na jamii inayowakaribisha, na inalenga masuala muhimu kwao wote - kutoka usalama hadi afya na elimu, au mabadiliko ya hali ya hewa.

> “Muundo wa tovuti ya uidhinishaji wa MCK hauwaainishi wanahabari kulingana na nchi wanamoishi au hadhi zao, bali kwa utaifa na kampuni ya habari ambayo mtu anafanyia kazi, kwa hivyo huenda iwe vigumu kufahamu kama mtu ni mwandishi wa habari mkimbizi au la,” (Mtoa habari muhimu, Mdhibiti wa Vyombo vya Habari)

# Mitindo katika mandhari ya vyombo vya habari

**Akiliunde (AI) inazidi kutumiwa** kuboresha vipengele vya utayarishaji, usambazaji na utumiaji wa habari nchini Kenya. Uelewa wa AI katika sekta ni mchanga, lakini unabadilika haraka, na washiriki walithibitisha kuwa wana ufahamu wa kiwango fulani wakati wa mahojiano. MCK imeweka kikosi kazi ili kuandaa miongozo ya vyombo vya habari kuhusu AI na Data.[xi]

**Kinyume na matarajio, mgawanyiko wa kidijitali unasalia.** Jamii za mijini, watu wa mapato ya kiwango cha kati, na jamii zenye kabila moja kubwa zinahudumiwa vyema sana. Jamii za makundi madogo, watu wa mashambani na watu maskini hawahudumiwi vizuri, na bado wanabeba mzigo mkubwa wa majanga na mabadiliko ya hali ya hewa. Kenya imepiga hatua kubwa katika huduma za TEKHAMA, ikiwa na usajili milioni 67.1 wa simu za mkononi katika watu zaidi ya milioni 54.[xii] Hata hivyo, sehemu nyingi za Kenya bado hazina ufikiaji wa huduma thabiti za simu, intaneti na data.[xliii] Ukosefu huu mbaya zaidi katika maeneo ya mbali kama vile kaunti 13 za Turkana, Mandera na Tana River ambapo ufikiaji wa mawimbi ya simu za mkononi unaweza kuwa umbali wa kutembea kwa zaidi ya kilomita mbili.

**Miji inaenda ya nchini Kenya inaendelea kukua navyo vyombo vya habari vinageuzwa kuwa vya kidijitali.** Wakazi wa mijini ni wapokezi wakubwa zaidi wa habari, mara nyingi wakiwa na mapato ya juu zaidi na ufikiaji mkubwa wa majukwaa ya kidijitali. Ufikiaji wa mtandao na teknolojia ya simu zimechochea matumizi ya vyombo vya habari vya kidijitali, hasa miongoni mwa wakazi wa mijini, ambao ndio watazamaji wengi zaidi.[xliii] .Vyombo vya habari vya jadi vimepanuka na sasa vinashirikiana na watazamaji kwenye majukwaa ya kijamii ya kidijitali na mtandaoni Asilimia 44% ya wanawake na 56% ya wanaume walikuwa wametumia mtandao katika miezi 12 iliyopita. Theluthi mbili ya wanawake na wanaume waliitumia kila siku. Miundomsingi ya mtandao ya uwezo wa mtandao kasi unaopatikana pia imeboreshwa[xlv] kwa asilimia 9.9% hadi Mbps milioni 12.0 mwaka 2022.[xlvi]

**Kumekuwa na ongezeko la uandishi wa habari wa kiraia mtandaoni.** Hali hii imesababisha usambazaji habari wa kidemokrasia, lakini inazua wasiwasi kuhusu usahihi na uaminifu wa maudhui ya habari. Pia kuna ongezeko la vyombo vya habari vya kienyeji ambavyo pia vinachukua sehemu kubwa katika kukuza vyombo vya habari nchini, likihakikisha kwamba hata wale walio mbali na kituo kikuu cha habari cha Nairobi bado wanaweza kupata habari katika lugha yao ya mama.

## Lugha na lahaja

**Lugha mbili rasmi nchini Kenya ni Kiingereza na Kiswahili.** Kuna zaidi ya lugha 60[xlvii] zinazozungumzwa kote nchini. Hii inajumuisha lugha za kienyeji na za kikabila ambazo zina lahaja tofauti. Uundaji na uwepo wa lugha anuwai ni msingi bora wa mandhari ya vyombo vya habari nchini, kumaanisha kwamba maudhui mara nyingi yanaundwa ili kukidhi makundi maalum ya lugha ili kuhakikisha ufikivu mpana wa habari na ushirikishaji wa jamii. Ingawa lugha hizo mbili rasmi zinatawala mawimbi ya utangazaji, vyombo vya habari pia hujumuisha lugha mbalimbali za kienyeji, zikiwemo, lakini sio tu, Kikuyu, Kiluhya, Kikalenjin, Kijaluo, Kikamba, Kisomali, Kisii, Mijikenda, Kimeru, Kimasai na Kiturkana. (tazama jedwali la 3 upate taarifa zaidi kuhusu lugha za utangazaji).

**Vituo vingi vya lugha za kienyeji vina ushawishi mkubwa**, hasa katika maeneo ya mashambani ambako lugha hizi huzungumzwa sana kama lugha ya kwanza. Stesheni za 'Sheng' [xlviii] za redio, kama vile Ghetto Radio, pia zimekuwepo hasa jijini Nairobi tangu mwanzoni mwa miaka ya 2000 na kuvutia hadhira ya vijana wa umri wa kati ya miaka 14 na 25, sio tu katika mji mkuu bali kote nchini. Kiswahili ni lugha inayopendelewa zaidi katika maeneo ya Pwani na Magharibi mwa nchi, huku usikilizaji wa stesheni za lugha za kienyeji ukiwa wa juu zaidi katika mikoa ya Mashariki ya Chini na Kanda ya Ziwa.

**Kiingereza na Kiswahili pia ndizo lugha zinazozungumzwa zaidi na wakimbizi** na[xlix] jamii nyingi, kando pamoja na Kiturkana (katika makazi jumuishi ya Kakuma na Kalobeyei) na Kisomali (katika kambi ya Dadaab). Huenda kusiwe na kikwazo kikubwa cha lugha wakati Kiswahili (75%) na Kiingereza (67%) kinapotumika pitisha taarifa kwa wakimbizi na jamii inayowakaribisha katika kambi ya wakimbizi ya Kakuma. Hata hivyo, haikuwa hivyo katika makazi jumuishi ya Kalobeyei, ambako hakuna lugha moja iliyotawala, huku Kiarabu kikiwa kimeenea zaidi kidogo. Turkana ndiyo maarufu zaidi (99%) kwa jamii ya mwenyeji katika eneo hilo.

**Ufikivu kwa watu wenye ulemavu umekuzwa na serikali.** Kwa mfano, Lugha ya Ishara ya Kenya (KSL) inakuzwa kama lugha ya kufundishia, mawasiliano, na ufikiaji taarifa kwa wale walio na matatizo ya kusikia. Vituo vingi, kama si vituo vyote vya televisheni nchini Kenya hutoa lugha ya ishara wakati wa matangazo ya habari na baadhi ya matangazo ya moja kwa moja. Baadhi ya vipindi vya televisheni hutoa chaguo za manukuu (ya kuona na kusikiliza) kwa watu wenye matatizo ya kuona na kusikia. Huku teknolojia saidizi ikiwa katika simu za mkononi, watumiaji wanaweza pia kupata vipengele vipya vya ufikivu na huduma zinazotegemea sauti ili kufikia maelezo. Teknolojia kama vile visoma skrini, programu ya kubadilisha maandishi kuwa usemi na vikuzaji vinasaidia ufikiaji wa maudhui dijitali. Mashirika kama vile Humanity & Inclusion huongeza ufahamu kuhusu watu wenye ulemavu mara nyingi baada ya kuanzisha mitandao ya mawasiliano ambayo wanaweza kutumia kufikia taarifa muhimu na zinazookoa maisha.

## Vizuizi vya kawaida vya ufikiaji

**Lugha hutumika kama daraja na vizuizi katika mfumo anuwai wa vyombo vya habari vya Kenya.** Katika muktadha wa wakimbizi, Dadaab hutumia sana lugha ya Kisomali kama lugha yao kuu ya utangazaji, huku Kakuma na Kalobeyei kwa kiasi kikubwa wakitumia lugha ya Kiturkana yenye mchanganyiko wa Kiswahili na Kiingereza katika lugha zao kuu za utangazaji. Hali hii inawafungia nje wakimbizi kadhaa wanaozungumza zaidi ya lugha nyingine 16 kutoka nchi nyingine. Lugha hizi ni pamoja na, lakini sio tu, Kidinka, Kinuer, Kiarabu, Kirundi, Kifaransa, Kibembe, Kididinga, Kiamhari na Kioromo. Lugha nyingine za walio wachache ni pamoja na Kiacholi, Kinari, Kibuya, Kifuliru, Kinyarwanda, Kirundi, Kilingala, Kilopit, Kilotuko, Kiluganda, Kimasalit, Kimashi, Kipalanda, Kizande, Kiajemi, Kipojulu na Kitigrinya. Chaguo za lugha katika utangazaji wa jamii husika na kitaifa huathiri ujumuishaji wa maudhui ya habari, hasa kwa vikundi vilivyo hatarini, vilivyotengwa, na watu wasiojua kusoma na kuandika.

**Hali za kijamii na kiuchumi huchangia katika tofauti za ufikiaji wa habari.** Gharama kubwa za bidhaa na huduma ni kikwazo kikubwa cha ufikiaji wa habari na vyombo vya habari. Washiriki wa mwongozo huu walitaja malipo, ulinzi, kijiografia, bei ghali ya vifurushi vya data na mapato ya chini kuwa vizuizi vya kufikia habari dijitali.

**Masuala ya Jiografia na tofauti za mijini na vijijini zinachangia utofauti unaosababishwa na habari.** Kadiri ulivyo maskini na ulivyo mbali na kituo cha habari (Nairobi) ndivyo ukosefu wa miundomsingi na vifaa unavyokuwa mkubwa, hasa katika maeneo ya vijijini. Miundomsingi duni ya barabara, kwa mfano, inatatiza usambazaji wa magazeti kutoka vyumba vya uchapishaji katika mji mkuu wa Nairobi, kwa sababu magazeti yanasafirishwa kwa magari. Matatizo ya miundomsingi ni pamoja na masafa finyu ya redio na umeme unaopotepotea.

**Viwango vya kujua kusoma na kuandika, jinsia na ulemavu huathiri ufikiaji wa habari na vyombo vya habari**. Asilimia 91% ya wanawake na 94% ya wanaume nchini Kenya wanajua kusoma na kuandika. Walio na elimu zaidi ya sekondari wanawakilisha 19% ya wanawake na 21% ya wanaume, wakati 6% ya wanawake na 3% ya wanaume hawana elimu. Kwa ujumla kuna viwango vya chini vya kujua kusoma na kuandika miongoni mwa wakimbizi na watu waliohamishwa kwa nguvu nchini. Watu wenye ulemavu wanaweza pia kutengwa kwa kuwa habari katika miundo maalum haipatikani kila wakati.

**Kuelewa vizuizi ni muhimu ili kuweza kuunda mikakati ya mawasiliano ambayo inaziba mapengo** na kuhakikisha taarifa zinafika kila pembe ya nchi — kuanzia jamii za wafugaji katika maeneo kame yenye ufikiaji mdogo wa redio, hadi kwa vijana wa mijini wanaoshuhudia mandhari ya kidijitali ya kasi.

> "Twitter, kwa maoni yangu, hutoa nafasi wazi ya mazungumzo ambapo watumiaji hukagua jumbe za uwongo katika sehemu za maoni na hata hutumia roboti za AI kubaini na kuripoti ukweli. Habari potofu, uwongo na hata matamshi ya chuki hivi majuzi, huwekewa alama nyekundu kila wakati. Licha ya kwamba hutumiwa zaidi kama kazi ya sanaa na chombo cha ushiriki wa kisiasa, inasalia kuwa jukwaa kubwa zaidi la habari. Kumbukumbu huhifadhiwa na habari inaweza kukumbukwa na kuchimbuliwa kwa urahisi."
> (Mtoa Taarifa Mkuu, INGO)

## Taarifa potofu na za uwongo

**Kizuizi kikuu pia ni uenezaji wa habari potofu na habari za uwongo katika Mandhari ya Vyombo vya Habari vya Kenya.** Habari za uwongo (24%), upendeleo (20%), na utangazaji duni wa masuala muhimu (14%)[ii] ni masuala makuu yanayoathiri mifumo ya utumiaji wa vyombo vya habari nchini Kenya, kulingana na MCK. Ni dhahiri kutokana na janga la COVID-19 kwamba habari za uwongo, uvumi, na habari potofu huzidisha hofu, kuongeza mkanganyiko na kutoaminika kwa mamlaka na miundo ya jamii, na kwa hivyo kuzuia kutolewa kwa huduma saidizi. Matatizo ni pamoja na utoafauti wa ubora wa uandishi wa habari, kueneza habari za kusisimua, na ukosefu wa uthibitishaji wa ukweli. Baadhi ya vyombo vya habari vinajitahidi kuboresha uandishi wao wa habari kwa kuripoti uchunguzi wa kina kuhusu masuala ya kijamii na kiuchumi, kuwa kufanya ufuatiliaji wa siku ya pili.

**Uenezaji unaoendelea wa uvumi, upotoshaji, na habari za uwongo mtandaoni na nje ya mtandao huharibu viwango vya uaminifu vya watumiaji wa habari.** Hali inahdhihirika sana hasa katika nchi kama vile Kenya ambako mgawanyiko wa kisiasa na mivutano ya kikabila huchochewa kwa urahisi, na hivyo kuchochea mivutano inayohusishwa na mapengo ya habari. Licha ya watoa habari wakuu kutaja mitandao ya kijamii kama moja ya vyanzo vyao vikubwa vya habari, walikubali pia kuwa majukwaa ya mtandaoni pia ni tishio kubwa kwa kuchochea habari potofu na uwongo kwa sababu hakuna hatua kali zinazowekwa kudhibiti kile ambacho watu wanachapisha mtandaoni.

**MCK na Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP) nchini Kenya walizindua Mtandao wa iVerify wa Vituo vya Kuthibitisha Ukweli mwaka[lii] wa 2022** ili kutatua taarifa potofu zinazoongezeka nchini, ambayo ni hatua ya kusifiwa ambayo vyombo vya habari inapaswa kuiga. Leo, zana ya iVerify inasimamiwa na MCK chini ya jukwaa la kukagua ukweli la Media Observer kwa kuendelea kutoa maoni kwa vyombo vya habari, wanahabari na umma kuhusu vipengee vya maudhui ya kidijitali.

**MCK imekuwa ikipiga hatua muhimu katika suala hili.** Ili kuadhimisha Siku ya Redio duniani ya UNESCO tarehe 13 Februari, 2024, Baraza la Vyombo vya Habari nchini Kenya lilizindua klabu 12 za wanahabari kote nchini ili kutumika kama majukwaa ya kujifunza, kuchanganua, na kushirikiana na wataalamu wa vyombo vya habari, kulingana na malengo mapana ya kukuza uandishi wa habari kwa uwajibikaji na kuwawezesha wananchi kushirikiana na vyombo vya habari kwa njia yenye manufaa.

> "Mitandao ya kijamii inalemewa sana na uvumi na kampeni za uchafuzi wa majina. Hata hivyo, X ni chanzo bora cha habari ikilinganishwa na mitandao mingine.
> (Mtoa Taarifa Mkuu, Shirika la maendeleo ya Vyombo vya Habari)

## Mapendeleo na uaminifu


**Mapendeleo ya vyombo vya habari yanahusinana na hali ya kijamii na kiuchumi na utambulisho wa kitamaduni.** Mazingira hutofautiana sana, kuanzia matatu za kupendeza jijini Nairobi, ambapo redio hucheza nyimbo mpya zaidi, hadi mazingira ya kilimo ya Eldoret, ambapo wakulima hukusanyika karibu na redio za jamii.

**Uaminifu katika media ndio wa juu zaidi kwa TV** (33%), ikifuatiwa na redio kwa 32%.[liii] 55% ya wanawake na 60% ya wanaume hutazama televisheni, na 8% ya wanawake na 16% ya wanaume husoma gazeti kila wiki. Kwa ujumla, wanaume zaidi (12%) kuliko wanawake (5%) mara nyingi hutumia njia zote tatu. Royal Media Services (RMS) ina ukadiriaji wa kuaminika wa 62%. Sifa zake thabiti zinatokana na utangazaji wake wa kina na kujitolea kwake katika kutayarisha maudhui yanayoangazia tamaduni za wenyeji. Asilimia 13% ya waliohojiwa walisema kuwa wana imani na KBC, huku 10% wakiweka imani yao katika Standard Group.

### Kuamini mashirika ya media - 2022

MEDIA COUNCIL OF KENYA

Royal Media Services (62%) ndilo shirika la habari linaloaminika zaidi nchini Kenya. Hii inachangiwa na utandawazi wake mpana na ujanibishaji wa huduma zake ili kuendana na tamaduni za wenyeji. Asilimia nyingine 13 na 10% ya waliohojiwa walionyesha kuwa wanaamini KBC na Standard Group mahususi.




**Swali: Ni chombo gani cha habari unachokiamini zaidi kwa habari?**

Ripoti ya Hali ya Vyombo vya Habari 2022

Katika kambi za wakimbizi za Dadaab na Kakuma, washiriki walitaja Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), Idara ya Huduma za Wakimbizi (DRS)[lv] na FilmAid Kenya (FAK) kama vyanzo vya habari vinavyoaminika.

**Nini hujenga uaminifu?**

Ikiwa shirika la vyombo vya habari au chanzo cha habari kiliripotiwa (Ripoti ya Hali ya Vyombo vya Habari ya MCK 22)

- masuala muhimu na habari za eneo husika kuhusu watu wa eneo hilo
- ilisifika sana katika suala la kuripoti habari kwa muda mrefu
- uwepo wa habari zinazochipuka au za sasa.

# Vyombo vya Habari katika Makabiliano na Kujitayarishia Maafa

**Kenya inakabiliana na 'matatizo matatu ya kibinadamu':** ukame, mizozo ya muda mrefu ya wakimbizi na mafuriko. Takriban 80% ya ardhi yote inakabiliwa na hali ya ukame kwa sasa. Hii ni pamoja na kaunti za Garissa na Turkana, ambazo ni makao ya kambi za wakimbizi za Dadaab na Kakuma na Kalobeyei katikamakazi yaliyounganishwa (makazi ya wakimbizi na watafuta hifadhi waliofukuzwa kutoka nchi jirani tangu 1991). Kulikuwa na angalau wakimbizi 700,000 waliosajiliwa na wanaotafuta hifadhi nchini Kenya kufikia tarehe 31 Januari 2024, huku wengi wao (55%) wakitoka Somalia na Sudan Kusini (24%).[lvii] Ukame umezidisha migogoro inayotegemea rasilimali, na kuwafanya wanawake na watoto kuathirika zaidi. Aidha, karibu wakimbizi 25,000 katika kambi ya Dadaab na 100 katika kabi ya Kakuma pia walikuwa wameathiriwa na mafuriko kufikia Novemba 2023, hivyo kusababisha kuhama zaidi ndani ya kambi hizi. Mwitikio wa kibinadamu, ikiwa ni pamoja na mipango ya mawasiliano na upashanaji habari, unaratibiwa kupitia Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (UNOCHA) na mashirika yanayoongoza kwa maeneo yaliyoathiriwa (maji, usalama wa chakula, afya n.k).[lviii]

**Mkusanyiko wa vyombo vya habari katika maeneo ya mijini mara nyingi husababisha hali ya kuripoti inayoegemea upande mmoja ambayo inapendelea matukio ya mijini kuliko yale ya vijijini na maeneo ya mbali.** Tofauti hii ni dhahiri zaidi wakati wa majanga, ambapo matukio katika mazingira ya mijini hupokea habari zaidi ikilinganishwa na matukio ya vijijini. Kwa mfano, ingawa mafuriko katika jiji kuu yanaweza kutawala vichwa vya habari, tukio kama hilo katika kijiji cha mbali hupuuzwa. Likitangazwa, vyombo vya habari vikuu huangazia mwanzo wa maafa kisha kuruka haraka hadi kwenye "mada kuu" kutoa habari kuhusu kuripoti maafa kama kuhusu ukame wa muda mrefu katika baadhi ya maeneo kame na au makavu ya nchi.

**Vyanzo vikuu vya taarifa kwa watu walioathiriwa hutofautiana wakati wa majanga au hali za dharura, na hutegemea eneo na muktadha.** Vituo vikuu na vya kawaida kama vile televisheni, dijitali, redio na magazeti huchangia pakubwa katika kutoa taarifa na arifa zinazookoa maisha kwa wale wanaoishi mijini. Jambo hili halifanyiki kwa uhusu jamii zilizoathirika katika maeneo ya mbali yaliyotengwa, ambapo ufikiaji wa vyombo vya habari vya kitamaduni ni ndoto ambayo haijatimia. Redio ya jamii na taarifa za kusimulia huwa vyanzo vya habari wakati wa mizozo na majanga. Mitandao ya kijamii hutoa maoni tofauti wakati wa majanga kuhusu jinsi ya kutoa huduma bora zaidi na pia imewapa fursa wanahabari wa kiraia kuwezeshwa kusimulia habari zao binafsi.

**Vyombo vya habari vya maeneo husika, ambavyo ni vyombo vya habari vya jamii na vituo vya redio vya wakimbizi vinaunda sehemu muhimu ya asili na mwitikio wakati wa maafa.** Kando na kutekeleza jukumu lao kuu la kutoa taarifa za kuaminika, pia huwapa matumaini kwa wale walioathiriwa na majanga. Vituo hivi hufanyika kiunganishi kati ya watoa misaada na jamii. Mazoezi ya uratibu wa onyo la mapema na juhudi za usaidizi hufanywa kwa usaidizi mkubwa wa vituo vya redio vya jamii na wakimbizi kulingana na muktadha. Mwaka 2020 wakati wa mzuko wa COVID-19, uhamasishaji na usambazaji wa itifaki za usalama ulifanywa hasa kupitia vyombo vya habari vya kitamaduni, mitandao ya kijamii na miundo iliyopo ya jamii.

> "Mitandao ya jamii pia inafanya kazi vizuri, na pia habari simulizi, mikutano, viongozi wa vijiji na jamii. Tunahitaji kuangalia kila aina ya njia za usambazaji. Hatuwezi kusema njia moja ni bora zaidi, inategemea muktadha. Njia tofauti zinaweza kutumika kwa wakati mmoja na kuelekezwa kwa walengwa.
> (Mtoa habari muhimu, Shirika la Kibinadamu)

## Jinsi ya kutumia mwongozo huu kujiandalia na kukabiliana na maafa?

> "Ingekuwaje ikiwa kila mtu angejua hatua ya kufanya wakati wa maafa? Mawasiliano ni muhimu katika maafa yoyote... kujua ni nani ameathirika, wapi na jinsi wanavyoweza kufikiwa, na jinsi wanavyoweza kufikishiwa msaada."

> "Kasi na haraka ya ukabilianaji inapaswa kuwa jambo la kimsingi, na haipaswi kuanza kuangalia waandishi wa habari waliokuja ni kina nani, na ni wa vyombo gani vya habari, habari hii inahitaji kujulikana awali."

> "Unapaswa kuweza kutazama kwa haraka na kujua watu wanazungumza lugha gani na wanaweza kufikiwa vyema kwa njia gani... Huokoa wakati muhimu katika maafa."
> (Waongoze watoa habari wakuu)

**Jitayarishe kabla ya jambo la dharura:**

- Miongozo ya Mandhari ya Vyombo vya Habari inaweza kutoa taarifa muhimu na ushauri ili kuwezesha mawasiliano ya pande mbili na uratibu wakati wa mizozo.
- Kwa kuelewa mahitaji ya vikundi mbalimbali, serikali na watoa misaada wengine wanaweza kubadilisha huduma zao ili kuhakikisha kuna ujumuishaji kabla ya dharura kutokea.
- Kwa kuchanganua ufikiaji na mifumo ya utumiaji wa habari mapema, mapungufu ya mawasiliano yanaweza kutambuliwa na rasilimali kutengwa ili kushughulikia mapungufu haya.
- Kufikia watu waliotengwa na wenye uwakilishi mdogo wakiwemo wakimbizi, au wale wenye ulemavu, kunahitaji mipango ya makusudi mapema.

**Katika kipindi cha majanga:**

- Tumia mwongozo kurekebisha kwa ufanisi zaidi mikakati ya mawasiliano ili kufikia jamii zilizoathirika. Ni muhimu kujua ni vyombo gani vya habari vyenye nafasi bora zaidi ya kufikia makundi yaliyotengwa, kwa kuzingatia viwango vya uwezo wa kusoma na kuandika, na mapendeleo ya lugha.
- Mawasiliano ya haraka ili kuondoa uvumi au habari potofu ni muhimu, kama vile kujenga imani kwa hadhira, jambo ambalo linaweza kuwezeshwa kupitia kubuni mbinu za mawasiliano za njia mbili kupitia vituo asilia kwa hadhira lengwa.
- Jenga imani katika mazingira ya wakimbizi kupitia
  - viongozi wa jamii na washawishi wa kitamaduni, kabla, wakati na baada ya maafa yoyote
  - Kuwasikiliza viongozi wa maeneo husika kuhusu jinsi ya kutafsiri ujumbe muhimu na masuala ya kitamaduni
  - kutumia mikutano ya vijijini na redio za jkamii kwa usambazaji wa habari zinazohusiana na hatari
  - Kuhakikisha kwamba habari inatangazwa katika lahaja ya eneo husika
  - Kutafsiri maelezo katika lugha nyingine ili kufikia hadhira pana
  - Ushirikiano wa jamii ili kuhakikisha kuwa ujumbe unaeleweka. Hili linaweza kufanywa kupitia miundo ya jamii iliyopo, ikijumuisha viongozi (waliochaguliwa na wajamii wenyewe), vikundi vya vijana, vikundi vya wanawake au mashirika ya kijamii; Vituo vya habari, pamoja na redio au mitandao ya kijamii inayotumiwa na umma.

## Mawasiliano ya njia mbili na jamii

**Kutumia vyombo vya habari kuwezesha ushiriki wa pande mbili** huwapa wanajamii nafasi ya kutoa hoja, kushiriki maarifa na kuhusika kikamilifu katika michakato ya kufanya maamuzi wakati wa mizozo, majanga na kuhamishwa. Katika makazi ya vibanda yenye shughuli nyingi kama yale ya Nairobi, ambapo redio za jamii hukuza sauti za wenyeji, na katika pembe za mbali za Marsabit, ambapo vipindi vya kupiga simu moja kwa moja vya redio huunganisha jamii, vyombo vya habari hutumika kama njia muhimu ya maoni ya jamii. Majukwaa haya huiwezesha jamii zilizotengwa kuwa na sauti na kuchangia kikamilifu kitoa suluhu za kukabiliana na maafa. Ushirikiano huu pia unaweza kusaidia vyombo vya habari kuondoa upendeleo na kuzingatia unyeti kaika mizozo. Hata hivyo, tovuti kuu za habari (The Daily Nation na Standard) hazitoi mawasiliano ya njia mbili. Walitaja sababu za kifedha kama vile kuajiri wasimamizi kuwa gharama kubwa.

**Vipindi vya kupiga simu kupitia redio, simu, WhatsApp, SMS (kwa tafiti za jamii) na mikutano ya jamii, vilitajwa kuwa njia muhimu zaidi za mawasiliano ya njia mbili** wakati wa hali za dharura na majanga. Kupitia njia hizi, wanajamii wanaweza kuuliza maswali, kutoa maoni, na kubadilishana maarifa yao kuhusu usaidizi na juhudi za usaidizi, huku mitandao ya kijamii, wanahabari wa kiraia, na mbinu za kitamaduni za mawasiliano zikiwa na ufanisi zaidi.

**Kujihusisha katika mazungumzo haya huyawezesha mashirika ya usaidizi kurekebisha makabiliano yao kulingana na mahitaji na masuala mahususi ya jamii zilizoathiriwa.** Mashirika kama vile DW Akademie na FilmAid Kenya yanatumia mbinu shirikishi ya kutoa na kusambaza habari, ikihusisha jamii katika utangazaji anuwai, uzalishaji na usambazaji wa maudhui katika lugha nyingi. Mbinu hii jumuishi inaboresha mawasiliano, ushirikishaji jamii na uwajibikaji, na kuziwezesha jamii zilizoathirika kuwa washiriki katika suluhu za maisha salama na yenye afya.

## Fursa za maendeleo ya vyombo vya habari na mawasiliano katika mizozo

**Ujumuishaji na utofauti**

- Toa mafunzo kuhusu hisia za kitamaduni, mapendeleo ya lugha, jinsia, watu wenye ulemavu, watoto na usimulizi wa hadithi jumuishi ili kuhakikisha mitazamo tofauti inawakilishwa.
- Tume ya utafiti kuhusu upendeleo wa vyombo vya habari na maelezo kwa watoto walio chini ya umri wa miaka 14. Kuna habari finyu inayopatikana, lakini katika mazingira yanayozidi kuwa ya kidijitali zaidi, vijana wanafunzwa na kutumia vyombo vya habari.

**Uhuru wa vyombo vya habari**

- Kuhamasisha umma kupitia vipindi vya elimu ya habari zinazolenga wanahabari na umma. Kuzingatia ujuzi wa kufikiri kwa kina, ujuzi wa kidijitali na kuelewa jukumu la vyombo vya habari katika jamii ili kuboresha uelewa wa umma, kutetea ulinzi wa wanahabari na kuondoa taarifa potofu.
- Kusisitiza jukumu muhimu la vyombo vya habari katika kujiandalia maafa, kukabiliana na maafa na ushirikishwaji wa jamii, hivyo kuchangia ustahimilivu wa jamii kwa ujumla.
- Kutoa ufadhili wa ulinzi wa kisheria, mafunzo ya usalama na ulinzi, na kanuni za usalama wa mtandao/digital ili kuimarisha uhuru wa uandishi wa habari.

**Maendeleo ya vyombo vya habari vya jamii**

- Kuweka kipaumbele cha uimarishaji wa redio za jamii, ambazo ni majukwaa muhimu katika maeneo yaliyotengwa.
- Kutoa usaidizi wa kiufundi, fursa za ufadhili na kuwajengea uwezo wanahabari na watangazaji wa maeneo huska. Kuwapa uwezo wa kufanya mawasiliano ya njia mbili ya hadhira.
- Kupanua upatikanaji wa elimu ya juu vijijini. Kuna zaidi ya vyuo vikuu 70 nchini, na vingi vinatoa kozi za uandishi wa habari na mawasiliano, kama ilivyoainishwa katika kiambatisho kilicho hapa chini. Vyuo vingi pia vimeidhinishwa na MCK ili kuongeza fursa anuwai. Taasisi nyingi, hata hivyo, zimejikita katika majiji.

**Mafunzo ya habari dijitali**

- Kutoa mafunzo kuhusu usimulizi wa hadithi dijitali, usimamizi wa mitandao ya kijamii na utengenezaji wa utangazaji anuwai.
- Kuhakikisha fursa za mafunzo ya AI yanajumuisha vipimo vya maadili ya matumizi ya AI.
- Kuwawezesha wanahabari kwa kufanya uchanganuzi wa data na ustadi wa utazamaji ili kufichua hadithi zilizofichwa kwenye data na uboreshaji wa ripoti za kiuchunguzi.

**Mafunzo ya uandishi wa habari wa kimaadili**

- Kusisitiza uandishi wa habari wa kimaadili kupitia mafunzo ya kukagua ukweli, mbinu za uthibitishaji na kuzingatia viwango vya kitaaluma, ili kukabiliana na taarifa potofu na kuripoti kwa upendeleo.
- Kuzingatia ufikiaji unaolengwa kwa 'wanahabari wa kiraia' ili kuhimiza wazingatie viwango vya kitaaluma.

**Miradi shirikishi ya kuripoti**

- Kuhimiza ushirikiano kati ya vyombo vya habari kupitia mipango ya pamoja ya kuripoti ili kushughulikia changamoto za kawaida na kuchunguza mbinu bunifu za kusimulia hadithi, kukuza ushirikishaji maarifa na kujenga uwezo ndani ya tasnia.
- Kuhimiza ushirikiano wa baina na nchi kwa ajili ya kujifunza kati ya wanahabari wenza na uanzishaji maadili bora katika kanda mbalimbali.

**Mawasiliano katika mizozo**

- Kuhimiza uungwaji mkono zaidi kwa vyombo vya habari vya Kenya, hasa vyombo vya habari vya umma na vya kijamii, ili kuangazia majanga ya kibinadamu.
- Kutoa taarifa iliyotafsiriwa katika lugha zaidi ya moja (mashirika yaliyofanya hivi yaliaminika zaidi ikilinganishwa na yale ambayo hayafanyi hivyo)
- Kuboresha miundo ya jamii na washawishi wa kitamaduni – mtandaoni na nje ya mtandao – ili kuwasilisha habari kwa ufanisi (muhimu mahali ambapo unyeti wa kitamaduni ni muhimu.)
- Kuhakikisha mawasiliano yanatumia mbinu nyingi, ikiwa ni pamoja na analogi, kabla ya kuzimwa kwa intaneti au kushambuliwa kwa miundomsingi ya jamii.
- Kuwafunza wafanyakazi katika mawasiliano ya njia mbili na kuwasiliana na watu wenye ulemavu.
- Kurekebisha mikakati ya mawasiliano yenye sifa maalum za kitamaduni zinazohusishwa na jiografia, historia na mapendeleo ya hadhira iliyokusudiwa.

# Viambatisho

Jedwali la 1 **Vyombo vya Habari vya Wakimbizi**

| Vyombo vya Habari Maarufu vya Wakimbizi walio Dadaab, Kakuma na Nairobi | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Vyombo vya habari vya wakimbizi** | **Umiliki na ufadhili** | **Kiungo cha tovuti** | **Lugha** | **Aina ya vyombo vya habari** | **Mahali** | **Wakimbizi** | **Mpangishaji** |
| **Star FM** | Star Media Development Centre (SMDC) | https://starfm.co.ke/ | Somali | Redio | Eastleigh, Nairobi | 3% | 0% |
| **Radio Gargaar** | Star Media Development Centre (SMDC) | https://starfm.co.ke/ | Somali | Redio | Hagadera, Dadaab | Haijulikani | Haijulikani |
| **Radio Ata Nayece** | Ata Nayece Media Services Ltd. | https://kkcfke.org/competition-winner/atta-nayece-media-services-limited/ | Kiturkana, Kiswahili, Kiingereza, Kiarabu cha Juba | Redio | Kakuma | 59% | 98% |
| **Ref FM** | Ilianzishwa na Action Africa Help International (AAH-I) na REF FM Foundation. Kwa sasa inasimamiwa na FilmAid Kenya. | https://www.ref-fmkk.com/ | Kiingereza, Kiswahili, Kisomali, Kiarabu, Kianyuak na Kinuer | Redio | Kalobeyei, Kaunti ya Turkana | Haijulikani | Haijulikani |
| **Eastleigh Voice** | Haijulikani | https://eastleighvoice.co.ke/ | Kiingereza | Habari dijitali | Nairobi | Haijulikani | Haijulikani |
| **Dadaab FM** | VoA | HAMNA | Somali | Redio | Dadaab | Haijulikani | Haijulikani |
| **Kakuma FM** | VoA | HAMNA | Kiingereza, Kiswahili, Kisomali | Redio | Kakuma | Haijulikani | Haijulikani |
| **Kanere.org** | Wakimbizi | https://kanere.org/about-kanere/ | Kiingereza | Habari dijitali | Kakuma | Haijulikani | Haijulikani |
| **Julisha.info** | Kibao cha Matangazo | https://www.julisha.info/en-us | Kiingereza, Kisomali, Kiswahili, Kiarabu | Habari dijitali | Kitaifa | Haijulikani | Haijulikani |
| **Bibilia Husema** | Wamishenari Bob na Lillian Davis wa Africa Inland Mission (AIM) | Biblia Husema Broadcasting | Kiswahili | Redio | Nairobi | 4% | 0% |

Jedwali la 2 **Habari Dijitali**

| Tovuti za habari zinazotembelewa zaidi | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Habari dijitali kuu** | **Umiliki na ufadhili** | **Lugha** | **Aina ya vyombo vya habari** | **Mahali** |
| **Tuko.co.ke** | Genesis Media Group of Companies | Kiingereza | Kibiashara | 28% |
| **Citizen.digital** | Royal Media Services | Kiingereza | Kibiashara | 22% |
| **Nation.Africa** | Nation Media Group | Kiingereza | Kibiashara | 15% |
| **Standardmedia.co.ke** | Standard Media | Kiingereza | Kibiashara | 13% |
| **Mpasho** | Radio Africa Group | Kiingereza | Kibiashara | 6% |

Chanzo cha jedwali: Baraza la Vyombo vya Habari nchini Kenya (2023)

Jedwali la 3 **Lugha za Utangazaji**

| Inajumuisha Lugha Rasmi na Lugha Nyingine Zinazotumiwa Hasa Katika Utangazaji | | |
|---|---|---|
| **Lugha ya utangazaji** | | **Idadi ya watu kwa makabila** |
| Lugha rasmi | Kiingereza | Haijaonyeshwa katika data |
| | Kiswahili | Haijaonyeshwa katika data |
| Lugha zingine | Kikuyu | 17.1% |
| | Kiluhya | 14.3% |
| | Kikalenjin | 13.4% |
| | Kijaluo | 10.7% |
| | Kikamba | 9.8% |
| | Somali | 5.8% |
| | Kikisii | 5.7% |
| | Kimijikenda | 5.2% |
| | Kimeru | 4.2% |
| | Maasai | 2.5% |
| | Kiturkana | 2.1% |
| | Sheng | Haijulikani |

Chanzo cha jedwali: CIA World Factbook.

Jedwali la 4 **Magazeti/machapisho yaliyosomwa zaidi**

| Gazeti la Daily Nation, Standard na gazeti la Kiswahili la Taifa Leo ndiyo machapisho yanayosomwa zaidi | | | |
|---|---|---|---|
| **Vyombo vikuu vya habari vya magazeti** | **Umiliki** | **Aina ya vyombo vya habari** | **Mahali** |
| **Daily Nation** | NMG | Kiingereza na Kiswahili | 53% |
| **The Standard** | Standard Media Group | Kiingereza | 22% |
| **Taifa Leo** | NMG | Kiswahili | 15% |
| **Star** | Radio Africa Group | Kiingereza | 3% |
| **Nairobian** | Standard Media Group | Kiingereza | 2% |
| **Business Daily** | NMG | Kiingereza | 2% |
| **People Daily** | Mediamax Network | Kiingereza | 1% |
| **Citizen Weekly** | Wachapishaji wa Vyombo vya Habari | Kiingereza | 1% |
| **The East African** | NMG | Kiingereza | 0.4% |
| **My Gov** | Serikali | Kiingereza | 0.4% |
| **New Vision** | The Vision Group | Kiingereza | 0.1% |

Chanzo cha jedwali: Ripoti ya MCK ya Vyombo vya Habari ya Kenya (2023)

Jedwali la 5 **Vituo Maarufu vya Redio nchini Kenya Kulingana na Hadhira: 2023**

| Vituo Vikuu vya Redio | Umiliki na Ufadhili | Lugha | Matangazo ya utumishi wa umma/jamii ya kibiashara | Ukifikiaji wa kidemografia | Vipindi maarufu zaidi |
|---|---|---|---|---|---|
| Radio Citizen | RMS | Kiswahili | Jamii ya kibiashara | 35+ | Vipindi vya Asubuhi na Nyakati za Usafiri |
| Radio Maisha | The Standard Group | Kiswahili | Jamii ya kibiashara | Umri wa miaka 25-34 | Vipindi vya Nyakati za Usafiri |
| Radio Jambo | Radio Africa Group | Kiswahili | Jamii ya kibiashara | Umri wa miaka 25-34 | Vipindi vya Usafiri wa Asubuhi na Jioni |
| Classic 105 | Radio Africa Group | Kiingereza | Jamii ya kibiashara | Umri wa miaka 25-34 | Vipindi vya Usafiri wa Asubuhi na Jioni |
| Milele FM | Mediamax Network | Kiswahili | Jamii ya kibiashara | 35+ | Vipindi vya Jumapili na vya Usafiri |
| Kiss FM | Radio Africa Group | Kiingereza | Kibiashara | Umri wa miaka 15-24 | Jioni |
| KBC English Service | KBC | Kiingereza | Utangazaji wa huduma kwa umma | Haijulikani | Evening Sundowner |
| Ramogi FM | RMS | Kijaluo | Kibiashara | Haijulikani | Asubuhi |

Chanzo cha jedwali: GeoPoll (2023)

Jedwali la 6 **Vituo vinavyotazamwa zaidi: 2023**

| Vituo Vikuu vya Televisheni | Umiliki na Ufadhili | Lugha | Matangazo ya utumishi wa umma/jamii ya kibiashara | Ukifikiaji wa kidemografia | Kipindi maarufu zaidi |
|---|---|---|---|---|---|
| Citizen TV | RMS | Kiingereza, Kiswahili | Kibiashara | 35+ | Taarifa za Saa 3 Jioni |
| NTV | Nation Media Group | Kiingereza, Kiswahili | Kibiashara | Haijulikani | Taarifa za Saa 3 Jioni |
| KTN Home | The Standard Group | Kiingereza, Kiswahili | Kibiashara | 25-34 | Taarifa za Saa 3 Jioni |
| KBC | Inamilikiwa na Serikali | Kiingereza, Kiswahili | Utangazaji wa huduma kwa umma | 35+ | Taarifa za Saa 3 Jioni |
| Inooro TV | RMS | Kikuyu | Kibiashara | 35+ | Haijulikani |
| Akili Kids | Akili Network | Kiingereza, Kiswahili, Lugha za Kijamii | Kibiashara | 0-17 | Saa 12 asubuhi hadi saa 3 usiku |

Chanzo cha jedwali: Baraza la Vyombo vya Habari nchini Kenya (2023)

Jedwali la 7 **Takwimu za Kulipia Vituo vya Habari nchini Kenya: 2023/2024**

| Kiashiria/Kipindi | | Septemba 2023 |
|---|---|---|
| Televisheni ya Upeperushaji Dijitali (DTT) | Go TV | 2735461 |
| | Star Times | 1741365 |
| | **Jumla Ndogo** | **4476826** |
| Moja kwa Moja Hadi Nyumbani (DTH) | Azam | 73758 |
| | MultiChoice (DSTV) | 1137898 |
| | Star Times | 304610 |
| | Wananchi (Zuku) | 285404 |
| | **Jumla Ndogo** | **1801670** |
| Cable | Cable One | 2658 |
| | CTN (MSA) | 2048 |
| | Wananchi (Zuku) | 56230 |
| | Hirani | 3600 |
| | Matrucchaya | 0 |
| | Wadani Cable | 95 |
| | **Jumla Ndogo** | **64631** |
| Jumla | | **6343127** |

Chanzo cha jedwali: CAK (2023/2024)

Jedwali la 8

| Vyuo vikuu, vitivo na vyuo vya elimu ya juu vinavyotoa kozi za uandishi wa habari, utangazaji, mawasiliano | | | |
|---|---|---|---|
| **Taasisi ya mafunzo** | **Mahali** | **Umiliki** | **Kozi ya/za kufuzu zinazotolewa** |
| **Chuo Kikuu cha Nairobi** | Juja, Kaunti ya Kiambu | Chuo cha Umma | Diploma, Shahada, Uzamili na PhD katika Mawasiliano ya Habari; Uandishi; Mahusiano ya Umma; Mawasiliano ya Makampuni na kozi nyinginezo |
| **Chuo Kikuu cha Kenyatta** | Athi River, Kaunti ya Machakos | Chuo cha Kibinafsi | Diploma ya TEKNOHAMA, Diploma ya Muziki, Mawasiliano, Shahada, Uzamili, na PhD katika Mawasiliano |
| **Chuo Kikuu cha Jomo Kenyatta cha Kilimo na Teknolojia** | Nairobi | Chuo cha Kibinafsi | Shahada ya Uandishi wa Habari; Shahada ya Utayarishaji na Uelekezaji wa Filamu; Uzamili katika Masomo ya Mawasiliano |
| **Chuo Kikuu cha Daystar** | Eldoret | Chuo cha Umma | Diploma ya Uandishi wa Habari wa Kifasihi; Shahada na Uzamili katika Isimu, Vyombo vya Habari na Mawasiliano; BSc na MSc katika Uandishi wa Habari na Vyombo vya Habari; Masomo ya Filamu na Vyombo vya Habari Uzamili; MSc. Katika Mafunzo ya Mawasiliano; PhD katika Mawasiliano na Uandishi wa Habari |
| **United States International University (USIU)** | Magadi Road-Ongata Rongai, Kaunti ya Kajiado | Chuo cha Umma | Diploma ya mwaka 1 ya Uandishi wa Habari; Mahusiano ya Kimkakati ya Umma na Filamu; Uhuishaji |
| **Chuo Kikuu cha Moi** | Nairobi | Chuo cha Kibinafsi | Shahada katika Mawasiliano (Uandishi wa Habari na Mahusiano ya Umma/ Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Maendeleo) |
| **Multimedia University of Kenya** | Mwembere Road, South B, Nairobi | Chuo cha Umma | Uandishi wa Habari Halisi; Uandishi wa Habari wa Matangazo; Utangazaji na Mahusiano ya Umma; Utayarishaji wa Vipindi vya Televisheni; Utayarishaji wa Vipindi vya Redio; Utayarishaji wa Vipindi vya Filamu/Video; Teknolojia ya Vyombo vya Habari; na nyingine nyingi |
| **Chuo Kikuu cha Strathmore** | Nairobi | Chuo cha Umma | Diploma ya Mawasiliano na Mitandao ya Kompyuta; Maktaba ya Diploma na Sayansi ya Habari; Ubunifu na Mawasiliano ya Diploma Graphics; Shahada ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma |
| **Kenya Institute of Mass Communication (KIMC)** | Kisumu | Chuo cha Umma | Cheti na Diploma ya Uandishi wa Habari na Vyombo vya Habari; Shahada ya Lugha na Mawasiliano na TEHAMA; Uzamili wa Isimu; Fasihi; Mafunzo ya Mawasiliano na Vyombo vya Habari n.k |
| **Technical University of Kenya (TUK)** | Nairobi | Chuo cha Kibinafsi | Kozi za Cheti, Shahada na Uzamili katika uandishi wa habari, mahusiano ya umma, uhuishaji na picha mwendo, masomo ya filamu, vyombo vya habari na mawasiliano, mawasiliano ya kampuni, na usimamizi wa vyombo vya habari. |
| **Chuo Kikuu cha Maseno** | Nairobi | Chuo cha Kibinafsi | Diploma ya Uandishi wa Habari; Shahada ya Uandishi wa Habari na Utangazaji Anuwai |
| **Chuo Kikuu cha Mt Kenya** | Kiambu | Chuo cha Kibinafsi | Diploma ya Mawasiliano ya Utangazaji |
| **Chuo Kikuu cha Riara** | Caxton House, Nairobi CBD | Chuo cha Kibinafsi | Cheti katika Utangazaji Anuwai; Diploma ya Uandishi wa Habari za Dijitali; Diploma ya Filamu na Utayarishi wa Televisheni nk |

Jedwali la 8 kuendelee

| Vyuo vikuu, vitivo na vyuo vya elimu ya juu vinavyotoa kozi za uandishi wa habari, utangazaji, mawasiliano | | | |
|---|---|---|---|
| **Taasisi ya mafunzo** | **Mahali** | **Umiliki** | **Kozi ya/za kufuzu zinazotolewa** |
| **Nairobi Institute of Business Studies (NIBS)** | Kiambu | Chuo cha Kibinafsi | Diploma ya Mawasiliano ya Utangazaji |
| **Africa Digital Media Institute (ADMI)** | Caxton House, Nairobi CBD | Chuo cha Kibinafsi | Cheti katika Utangazaji Anuwai; Diploma ya Uandishi wa Habari za Dijitali; Diploma ya Filamu na Utayarishi wa Televisheni nk |
| **Chuo Kikuu/ Kitivo cha Zetech** | uzalishaji nk | Chuo cha Kibinafsi | Shahada (Shahada ya Sanaa) katika Mawasiliano ya Kijamii, Diploma ya Utayarishi wa Vyombo vya Habari, Cheti cha Utayarishi wa Vyombo vya Habari. |
| **Chuo Kikuu cha Tangaza** | Kwenye Bararaba ya Thika Road, Ruiru | Chuo cha Kibinafsi | Cheti cha Uandishi wa Habari; Diploma ya Uandishi wa Habari |
| **Aga Khan Graduate School of Media and Communications** | Langata South Road, Nairobi | Chuo cha Kibinafsi | Shahada (Shahada ya Sanaa) katika Mawasiliano ya Kijamii, Diploma ya Utayarishi wa Vyombo vya Habari, Cheti cha Utayarishi wa Vyombo vya Habari. |
| **Chuo Kikuu cha Karatina** | Nairobi | Chuo cha Kibinafsi | Vyombo vya Habari na Mawasiliano, Uzamili wa Uandishi wa Habari Dijitali |
| **Chuo Kikuu cha Rongo** | Migori | Chuo cha Umma | Mawasiliano |

Jedwali la 9

| Mashirika ya Maendeleo ya Vyombo vya Habari yanayotoa Mafunzo ya Uandishi wa Habari kwa Wakimbizi nchini Kenya | | | |
|---|---|---|---|
| **FilmAid Kenya** | Nairobi, Kakuma na Dadaab | Shirika Lisilo la Serikali | Mafunzo ya Vyombo vya Habari na Ujasiriamali, Warsha za Vyombo vya Habari, Sanaa za Ubunifu na Mafunzo ya Kujieleza |
| **Internews Network** | Nairobi, Washington DC, Uingereza na Ufaransa | Shirika lisilo la faida la Kimataifa la Usaidizi wa Vyombo vya Habari | Mafunzo ya Uandishi wa Habari, Maendeleo ya Vyombo vya Habari, Huduma za Habari za Kibinadamu |
| **DW Akademie** | Ujerumani | Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Vyombo vya Habari | Mafunzo ya Uandishi wa Habari, Usambazaji Maarifa |

Kumbuka: katika baadhi ya matukio, hili linajumuisha ushirikiano na taasisi nyingine zilizoidhinishwa ili kutoa vyeti vya kitaaluma

# Maelezo ya Mwisho

[i] Vyombo vikuu vya habari, hasa kutoka Mataifa Matajiri ya Ng'ambo, ni nadra kutoa habari za kina kuhusu masuala muhimu katika kambi za wakimbizi nchini Kenya. "Vyombo hivi vinapoangazia kambi hizi, wakimbizi ni nadra sana kuulizwa maoni yao kando na hali yao ya sasa; jambo linalozidisha mtazamo wa wakimbizi kuwa kundi kubwa la wahasiriwa wanaokabiliwa na njaa na wasio na matumaini" (chanzo: Jarida la Media Perception lililochapishwa na JSTOR.org)
[ii] Tafiti za mtandaoni zilitumika zaidi kwa watoa taarifa wakuu katika maeneo yenye muunganisho duni. Jumla ya watu 138 walifikiwa kupitia mbinu hizi katika muda wa wiki tatu, na hati 27 kukaguliwa.
[iii] C. Ombati (2024) Security alert in Mandera as gunmen destroy communication mast, The Star, 12 Januari.
[iv] D. Kiereini (2021) Tracing history of KBC and evolution of broadcasting, Business Daily, 21 Mei.
[v] Kenya National Bureau of Statistics (2022) Ripoti ya Uchambuzi ya Sensa ya Watu na Makazi ya 2019 kuhusu Makadirio ya Idadi ya Watu, Hazina ya Kitaifa na Mipango, Septemba.
[vi] ReelAnalytics (2022) Ripoti ya Hali ya Vyombo vya Habari.
[vii] Benki ya Dunia (n.d.) Afrika Mashariki na Kusini: Habari za maendeleo, utafiti, data, ukurasa wa wavuti.
[vii] Sheria katika Katiba ya Kenya inatoa hakikisho kwamba kila raia ana haki ya kupata taarifa inayomilikiwa na Serikali au mawakala wake, iwe wako katika utumishi wa kiraia au wa umma; na taarifa iliyo na mtu mwingine inayohitajika kwa ajili ya kutekeleza au kulinda haki yoyote au uhuru wowote wa kimsingi. Tume ya Kitaifa ya Kenya ya Haki za Kibinadamu (n.d.) Access To Information Request, ukurasa wa tovuti.
[ix] Reporters Without Borders (n.d.) Kenya, ukurasa wa tovuti.
[x] G. Marete & D. Machui (2024) Seventh suspect arrested in Meru blogger Sniper's murder probe, Nation, 8 Januari.
[xi] Baraza la Vyombo vya Habari nchini Kenya [@MediaCouncilK] (2024) "Redress: @MediaCouncilK seeks court intervention for journalists' compensation. Kupitia .@StandardKenya More: https://t.co/vE8XuJ31FJ #MCKInTheNews", X, 6 Februari.
[xii] Global Disinformation Index (2021) Tathmini ya Hatari ya Usambazaji Habari Potovu: Soko la Habari za Mtandaoni nchini Kenya,.
[xii] People Daily (2024) Remunerate journalists well, Media Council urges employers, Februari 12.
[xiv] Gazeti la serikali lililo na zabuni na mawasiliano yote ya serikali, ikijumuisha habari kutoka wizara tofauti.
[xv] https://kenyalaw.org/kl/fileadmin/pdfdownloads/Acts/2021/TheRefugeesAct_No10of2021.pdf
[xvi] Utafiti wa kitaifa uliofanywa na Mamlaka ya Mawasiliano (The Communication Authority) mwezi Julai hadi Oktober 2023 https://www.ca.go.ke/sites/default/files/2024-02/Audience%20Measurement%20and%20Industry%20Trends%20Report%20July-September%202023_0.pdf
[xvii] Tofauti na redio za kibiashara, redio za kijamii zinamilikiwa na kuendeshwa na wanajamii wa eneo husika, kukuzwa kwa ushirikiano na wanajamii, na masafa ya utangazaji wao kawaida unalenga eneo mahususi la kijiografia ambapo jamii hiyo inaishi.
[xvii] Baraza la Vyombo vya Habari nchini Kenya [@MediaCouncilK] (2024) "Mandhari ya Vyombo vya Habari nchini Kenya yamebadilika sana...",, X
[xix] Sampuli ya muundo wa KDHS ya 2022 hutoa makadirio katika kiwango cha kitaifa, kwa maeneo ya mijini na mashambani, na kwa baadhi ya viashiria kwa kila kaunti 47 za Kenya. Sampuli wakilishi ya kitaifa ya wanawake 32,156 wa umri wa miaka 15-49 katika familia 37,911 na wanaume 14,453 wa umri wa miaka 15-54 katika nusu ya familia zilizochaguliwa walihojiwa. Hii inawakilisha kiwango cha mwitikio cha 95% ya wanawake na 87% ya wanaume.
[xx] Kenya National Bureau of Statistics (2022) Utafiti wa Kidemografia na Afya wa Kenya.
[xxi] F. Kibuacha (2024) Kenya Media in 2023 - Top TV and Radio Shows, GeoPoll, 8 Februari.
[xxii] Tathmini ya Hadhira za Vyombo vya Habali Nchini Kenya Mwaka 2023
[xxiii] Internews (n.d.) Kenya – Refugees in Dadaab (2012-2016), ukurasa wa wavuti.
[xxiv] Internews (2020) In Kenya, Providing Refugees with Life-Saving Information about COVID-19 and Other Health Issues, 27 Aprili.
[xxv] Julisha.info (2021) Tune into 'Bilan' and 'Sauti ya Mwanamke' radio shows: reliable infomraiton in Dadaab and Kakuma.
[xxvi] Kanere (2021) VoA Commences FM Radio Stations for Refugees, 3 Februari.
[xxvii] Kulingana na Ripoti ya Takwimu ya Sekta ya Robo ya Kwanza ya CAK katika kipindi cha tarehe 1 Julai hadi 30 Septemba 2023.
[xviii] Baraza la Vyombo vya Habari nchini Kenya (2023) Vituo vya Televisheni Vilivyotazamwa Zaidi Mwaka 2023.
[xxix] S. Maombo (2023) Radio Africa shuts down Kiss TV, NTV, 17 Machi.
[xxx] Ripoti ya Baraza la Vyombo vya Habari nchini Kenya (MCK) ya Hali ya Vyombo vya Habari nchini Kenya 2022
[xxx1] Data ya utafiti wa kitaifa uliofanywa na Mamlaka ya Mawasiliano
[xxxii] Kenya National Bureau of Statistics (2022) Utafiti wa Kidemografia na Afya wa Kenya,
Ripoti ya takwimu za sekta ya robo ya kwanza ya Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya (CAK) kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024
[xxxiv] Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya (2024) Register of Unified Licensing Framework Licensees, Januari.
[xxxv] Takwimu za Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya ya FY 2023/2024 inaonyesha Safaricom PLC na Telkom Kenya Ltd zilipoteza sehemu zake za soko katika usajili wa simu za mkononi (SIM) na mtandao kasi huku Airtel Networks ikipata ongezeko katika maeneo yote mawili.
[xxxvi] Mkakati wa Kitaifa wa Mtandao Kasi 2018-2023 unafafanua Mtandao Kasi kuwa muunganisho unaotoa huduma shirikishi, salama, za ubora na nafuu kwa kasi isiyongua Mbps 2. Mtandao Kasi wa mkononi unajumuisha 3G, 4G na 5G.
[xxxvii] A. Njanja (2019) Facebook sets up content hub in Nairobi, Business Daily, 7 Februari.
[xxxviii] Facebook Content Moderators Sue Meta in Kenya | TIME Machi 2023

[xxxix] Mfano mmoja wa mitindo ya kidijitali inayoibuka kuhusu utoaji wa taarifa katika mazingira ya hali za dharura ni Julisha.info - ambalo ni tawo la Signpost, mradi wa mashirika yanayoongozwa na IRC, ambao huunda vituo vya usaidizi vya kidijitali.
[xl] Baraza la Vyombo vya Habari nchini Kenya (2023) MCK Unveils Taskforce on Data and AI Guidelines,, 24 Oktoba.
[xli] iliyorekodiwa katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha wa 2023/2024, kwa mujibu wa CAK
[xlii] Jamhuri ya Kenya (2018) National Broadband Strategy 2018-2023.
[xliv] Kenya National Bureau of Statistics (2022) 2019 Sensa ya Idadi ya Watu na nyumba.
[xlv] Kwa mujibu wa Ripoti ya Takwimu ya Robo ya Kwanza ya Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 ya Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya, sekta ya TEHAMA ya Kenya iliendelea kuonyesha mwelekeo wa juu katika utumiaji wa huduma za simu, ikichochewa na maendeleo katika uunganisho wa simu za mkononi na upatikanaji wa miundomsingi. Kwa hivyo, hali hii imesababisha miunganisho ya haraka na ya kuaminika zaidi.
[xlvi] Kenya National Bureau of Statistics (2022) Utafiti wa Kidemografia na Afya wa Kenya.
[xlvii] CIA World Factbook (2022) Kenya, 21 Desemba.
[xlviii] Sheng ni lugha ya mijini ya kipekee na inayobadilika au lugha ya mtaani inayozungumzwa sana nchini Kenya, hasa jijini Nairobi na maeneo mengine ya mijini. Ni mchanganyiko wa lugha mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Kiswahili, Kiingereza, na lugha za kijamii nchini Kenya, pamoja na vipengele vya utamaduni wa muziki wa hip-hop. Sheng hujumuisha maneno, vishazi, na misemo kutoka kwa lugha hizi, mara nyingi vikiunganishwa kwa ubunifu au kubadilishwa ili kutoa maana mahususi katika muktadha wa utamaduni wa vijana, maisha ya mijini, na mwingiliano wa kijamii. Inatumika kama aina ya utambulisho na usemi wa kitamaduni kwa vijana nchini Kenya, ikionyesha athari mbalimbali za lugha na tamaduni zilizopo katika mazingira ya mijini.
[xlix] DW Akademie (2021) Hakuna magazeti hapa: Information needs assessment among refugees and host communities in Ethiopia, Kenya and Tanzania.
[l] Kwa mujibu wa KDHS 2022
[li] Baraza la Vyombo vya Habari nchini Kenya (2023).
[lii] Baraza la Vyombo vya Habari nchini Kenya (2022) New Fact-checking Tool to Counter Fake News, 1 Julai.
[liii] Ripoti ya Hali ya Vyombo vya Habari 2022
[liv] Ripoti ya Hali ya Vyombo vya Habari ya Baraza la Habari la Kenya (2022).
[lv] DRS ni idara ya serikali inayosimamia masuala ya wakimbizi nchini. Idara hii inadhibiti usimamizi wa kambi za wakimbizi nchini Kenya.
[lvi] Mafuriko haya ya ghafla na maporomoko ya ardhi pia yameathiri pakubwa sehemu nyingine za nchi katika siku za hivi majuzi ikiwa ni pamoja na Kisumu, Mombasa na Tana River pekee.
[lvii] Takwimu za UNHCR
[lviii] OCHA (2012) OCHA kupitia Ujumbe: The Cluster Approach, Machi.
[lix] UNHCR (n.d.) Vipindi vya Redio, Help Kenya. ukurasa wa tovuti.

CDAC ni mtandao wa zaidi ya watendaji 35 wakubwa zaidi wa kibinadamu, maendeleo ya vyombo vya habari na uvumbuzi wa kijamii – ikiwa ni pamoja na mashirika ya Umoja wa Mataifa, RCRC, NGOs, vyombo vya habari na watendaji wa mawasiliano – wanaofanya kazi pamoja ili kubadilisha piga juu ya utoaji wa maamuzi ya kibinadamu na maendeleo – kutoka kwa kimataifa. kwa mtaa.

© CDAC Network 2024

**CDAC Network**
Sayer Vincent-Invicta House
108–114 Golden Lane
London EC1Y 0TL
Uingereza

cdacnetwork.org
@CDACN
@CDACN
CDAC Network
@CDACNetwork

Nambari ya Usajili wa Nyumba ya Makampuni: 10571501
Nambari ya Msaada Iliyosajiliwa: 1178168